zamani	long time ago
kesho	tomorrow
kesho kutwa	day after tomorrow ( <i>also keshokutwa</i> )

### *Hours, minutes, seconds*

saa	hour(s), clock(s), watch(es)
masaa	( <i>pl.</i> ) many hours
dakika	minute(s)
sekunde	second(s)
robo	quarter
nusu	half
kasoro	less
kasorobo	less a quarter ( <i>cf. kasoro robo; also kasorobo, kasarobo</i> )
saa tano na nusu	half past eleven ( <i>alternatively saa tano u nusu</i> )

<b>saa tatu na robo</b>	quarter past nine
<b>saa tatu kasorobo</b>	quarter to nine
<b>saa kumi na moja na dakika saba</b>	seven minutes past five

## Exercise 6

Write in English:

- 1 Treni kutoka Dodoma itafika saa moja na nusu jioni.
- 2 Treni kwenda Mbeya itaondoka saa saba kasorobo mchana.
- 3 Treni kutoka Tabora itafika saa tatu na dakika tano usiku.
- 4 Treni kwenda Morogoro itaondoka saa nne kasoro dakika kumi asubuhi.
- 5 Treni kutoka Moshi imeshafika saa moja na nusu asubuhi.

## Exercise 7

Your turn to be at the booking office. You and a friend want to buy rail tickets to go to Tanga. Below is a dialogue between the station clerk and yourselves. Translate the dialogue into Swahili:

YOU:	How are you this morning?
CLERK:	Just fine. You are welcome.
YOUR FRIEND:	Thanks. We want to go to Tanga. What price are the tickets?
CLERK:	The price for a first-class ticket is five hundred shillings. How many tickets do you want?
YOUR FRIEND:	We want two tickets.
CLERK:	The price is one thousand shillings.
YOU:	What time will the train leave?
CLERK:	The train will leave at 10 o'clock in the morning.
YOU AND FRIEND:	Thank you. Goodbye.
CLERK:	Goodbye. Have a nice trip!
YOU AND FRIEND:	Thanks a lot.

## Exercise 8

Write the times below in Swahili time:

- 1 9 a.m.; 10 a.m.; 11 a.m.; 3 p.m.; 4 p.m.; 5 p.m.
- 2 1.30, 2.45, 7.15
- 3 1 hour, 2 minutes and 3 seconds

## Dialogue 3

*Leo and Victoria are now discussing travel arrangements with fellow students, Subira and Trevor, who will accompany them on the journey*

- 1 The students will visit how many countries and in what order?
- 2 Approximately how long will the journey take?
- 3 Who offers to take the passports to the embassy?

TREVOR: Je, treni ina behewa la kulia chakula?

VICTORIA: Ndiyo, ina behewa la kulia chakula.

SUBIRA: Katika safari yetu, tutapitia nchi ngapi?

LEO: Tutapitia nchi nne: ya kwanza Zambia, ya pili Zimbabwe, halafu tutapita Msumbiji bila ya kusimama kuelekea Malawi. Baada ya kukaa Malawi, tutarudi Tanzania. Safari nzima itachukua muda wa karibu wiki nne.

TREVOR: Bila shaka safari kama hiyo itatupa elimu zaidi kuhusu mambo ya Afrika Mashariki.

LEO: Kuingia nchi hizo tutahitaji viza. Tutaweza kupata viza kwenye ubalizi. Kesho nitazichukua pasi kwenye ubalizi.

VICTORIA: Haya, tutakupa pasi.

TREVOR: Mimi ni Mkanada, kwa hiyo nina pasi ya Kanada.

SUBIRA: Nilizaliwa Kenya, kwa hiyo pasi yangu ni ya Kenya. Bibi Victoria, una utaifa gani?

VICTORIA: Mimi ni Mghana. Nina pasi ya Ghana. Bwana Leo, una utaifa gani?

LEO: Taifa langu ni Uingereza. Basi! Kanada, Kenya, Ghana na Uingereza sisi sote tunasafiri pamoja. Tutajiita 'Umoja wa Mataifa!'

TREVOR: *Does the train have a dining car?*

VICTORIA: *Yes, it has a dining car.*

SUBIRA: *How many countries will we visit during our trip?*

LEO: *We'll visit four countries: the first, Zambia, the second, Zimbabwe, and then we will pass non-stop through Mozambique on to Malawi. After staying in Malawi, we'll return to Tanzania. The complete journey will take a period of nearly four weeks.*

TREVOR: *Without doubt a trip like this will give us more knowledge about East Africa.*

- LEO: *To enter these countries we'll need visas. We will be able to get the visas at the embassy. Tomorrow I'll take the passports to the embassy.*
- VICTORIA: *Okay, we'll give you the passports.*
- TREVOR: *I'm Canadian, so I have a Canadian passport.*
- SUBIRA: *I was born in Kenya, so my passport is Kenyan. Miss Victoria, what nationality are you?*
- VICTORIA: *I'm Ghanaian. I have a Ghanaian passport. Mister Leo, what is your nationality?*
- LEO: *My nationality is British. Well then! Canada, Kenya, Ghana and England, all of us travelling together. We shall call ourselves the 'United Nations!'*

## Vocabulary

<b>behewa</b>	train compartment or carriage
<b>-lia</b>	eat with or in ( <i>cf.</i> <b>-la</b> , eat)
<b>chakula</b>	food ( <i>so</i> , <b>behewa la kulia chakula</b> , carriage for eating food in)
<b>-pitia</b>	pass by/at/near, pay a passing visit
<b>nchi</b>	country(ies)
<b>bila (ya)</b>	without
<b>-simama</b>	stop, stand, stand up
<b>-elekea</b>	be headed for/going to, be facing (seem, appear, feel inclined)
<b>karibu</b>	nearly, near, nearby ( <b>karibu na</b> , near to) ( <i>cf.</i> <b>Karibu!</b> Welcome!)
<b>shaka</b>	doubt ( <b>bila shaka</b> , without doubt. <b>Hapana shaka</b> is <i>sometimes heard, meaning</i> 'No doubt')
<b>-pa</b>	give ( <i>used either with the stem marker ku-</i> , or with an object concord, discussed in Language structure below)
<b>elimu</b>	education
<b>-ingia</b>	enter
<b>-hitaji</b>	need
<b>viza</b>	visa(s)
<b>-pata</b>	get
<b>ubalozi</b>	embassy
<b>-chukua</b>	carry, take away
<b>pasi</b>	passport(s)
<b>utaifa</b>	nationhood
<b>taifa</b>	nation ( <i>pl.</i> <b>mataifa</b> )

<b>sisi sote</b>	all of us
<b>Umoja wa Mataifa</b>	the United Nations

## Language structure

### *The JI-MA noun class*

**Taifa** and **behewa** are, like **jina**, **nen**, and **jambo**, encountered in Unit 1, nouns belonging to the JI-MA noun class. The plural nominal prefix is **ma-**, so that nouns in this class in the plural begin with **ma-**, as for example **mabehewa**, ‘carriages’ and **mataifa**, ‘countries’. However, not all singular nouns in this class begin in **ji-** (as one would expect from the name of the class). In fact, only a few nouns do – mostly those with monosyllabic stems, that is nouns which consist of one syllable only if the nominal prefix is subtracted.

<i>Singular</i>	<i>Plural</i>	
<b>behewa</b>	<b>mabehewa</b>	carriage
<b>nen</b>	<b>manen</b>	word
<b>taifa</b>	<b>mataifa</b>	nation, nationality
<b>yai</b>	<b>mayai</b>	egg
<b>ji</b>	<b>maji</b>	eye

With some nouns, the plural becomes **me-**, when the vowels **a** and **i** fuse together to form **e**:

<b>jino</b>	<b>meno</b>	tooth
<b>jiko</b>	<b>meko</b>	stove, kitchen

These slightly irregular pairs also belong here:

<b>jina</b>	<b>majina</b>	name
<b>jambo</b>	<b>mambo</b>	matter

Some JI-MA nouns do not have a singular, they are only found in the plural:

<b>maziwa</b>	milk
<b>mafuta</b>	oil
<b>maji</b>	water

The possessive concord of the JI-MA class is of course **li-** and **y-**, already familiar from Unit 1. The concord for this class is **li-** in the singular and **ya-** in the plural.

**Behewa langu linapendeza.**

My carriage is pleasant.

**Mabehewa yangu yanapendeza.**

My carriages are pleasant.

**Yai liko wapi?**

Where is the egg?

**Mayai yako jikoni.**

The eggs are in the kitchen.

## Language structure

### *The object concord*

By now you have become quite familiar with the subject concord, which indicates which participant, person, or thing is the subject of the verb. The participant, person, or thing towards which an action is directed is called the object, and the object can be expressed in Swahili by the object concord, which precedes the verb stem:

<i>Subject concord</i>	<i>Tense</i>	<i>Object concord</i>	<i>Verb stem</i>	
<b>ni</b>	<b>ta</b>	<b>zi</b>	<b>chukua</b>	<b>nitazichukua</b> I will carry them ( <i>of an inanimate N-class plural noun</i> )
<b>tu</b>	<b>ta</b>	<b>ku</b>	<b>pa</b>	<b>tutakupa</b> we will give you ( <i>sing.</i> )

As can be seen from the examples above, the object concord follows the tense marker and precedes the verbal base. When the object is a participant or human, the object concord is generally used, while for non-human objects, the object concord is possible, but not necessary.

The object concords for participants are given below:

<b>ni</b>	me	<b>tu</b>	us
<b>ku</b>	you ( <i>sing.</i> )	<b>ku . . . ni</b>	you ( <i>pl.</i> )
		<i>or wa . . . ni</i>	
		<i>or just wa</i>	

For example with the verb **-ona**, 'see':

<b>aliniona</b>	he saw me
<b>walituona</b>	they saw us
<b>nitakuona</b>	I will see you ( <i>sing.</i> )
<b>nitakuoneni</b>	I will see ( <i>each of</i> ) you ( <i>pl.</i> )
<b>nitawaoneni</b>	I will see ( <i>all of</i> ) you ( <i>pl.</i> )
<b>nitawaona</b>	I will see ( <i>all of</i> ) you ( <i>pl.</i> )

The post-final **-ni** changes the final vowel (which is now strictly speaking no longer final) from **-a** to **-e**. This is the same **-ni** as we have seen in Unit 1 in **Asanteni**. There are three forms for the object concord for 'you (*pl.*)'. The first one, **ku . . . ni**, is more often used to refer to individuals in a group, while the second one, **wa . . . ni**, often refers to the group as a whole. The third one is identical to the plural object concord of the M-WA class:

<b>nitawaona</b>	<i>can mean</i>	I will see ( <i>all of</i> ) you ( <i>pl.</i> )
		<i>or I will see them.</i>

For these forms, the context makes clear what is meant.

For the singular of the M-WA class, the object concord is **-m-** (or, when followed by a vowel, **-mw-**); for all other classes, the concord is used, so that the object concord has the same shape as the subject concord. The object concord can be used with all tenses:

**Nilimwona mwenzangu.**

I saw my friend.

**Nitazikata tiketi hizi.**

I will buy these tickets.

**Utamwoa Mzambia mzuri.**

You will marry a beautiful Zambian.

**Hawajamwita.**

They have not yet called her/him.

**Mmeyakumbuka.**

You (*pl.*) have remembered them (*of a JI-MA plural noun*).

A special object concord **-ji-** exists for reflexive meanings, where an action is performed by somebody with reference to themselves:

**Tutajiita Umoja wa Mataifa.**

We will call ourselves United Nations.

**Alijikata.**

S/he cut herself/himself.

When used with monosyllabic verbs, the object concord replaces the stem marker:

**Nilizila.**

I ate them (*of an N-class noun*).

**Watayanywa.**

They will drink them (*of an JI-MA noun*).

**Anampa habari.**

He/she is giving him/her news.

## Exercise 9

Put the correct object marker into the gap in the sentences. Object markers: **zi, li, i, m, wa**:

- 1 Asha ali\_\_kata tiketi moja.
- 2 Nita\_\_pata habari za ubalozi kesho.
- 3 Je, ume\_\_ona watoto?
- 4 Wanafunzi wame\_\_pa Amos pasi zao.
- 5 Asha ali\_\_ona behewa la kulia.

## Exercise 10

- 1 How do you ask someone the time?
- 2 How do you ask someone the date?
- 3 How do you say the time is 3:25 p.m.?
- 4 How do you say the date is Tuesday, 18 January?

## Exercise 11

Write in English:

Ninakaa Marekani. Leo ninakwenda kukata tiketi ya kusafiri kwa ndege. Ninataka kwenda Afrika. Zamani baba yangu



alikuwenda Afrika. Alikwenda Uganda na Kenya. Jana nilipata viza yangu kwenda Tanzania. Kesho nitakwenda kwa baba yangu kupata habari zake kuhusu kusafiri Afrika. Ndege itaondoka kesho kutwa.

## Reading

### TAZARA

TAZARA ni reli kuu ya kuunganisha Dar es Salaam (Tanzania) na Kapiri Mposhi (Zambia), kupitia mpaka wa Tanzania–Zambia kati ya Tunduma na Nakonde. TAZARA inapitia sehemu ya mbuga ya wanyama ya Selous. Njia hiyo ya reli ilijengwa na Jamhuri ya Watu wa China katika miaka ya sitini. Vilevile kulikuwa na ujenzi wa stesheni mia moja na arobaini na saba, zaidi ya daraja mia tatu na mashimo ya kupenya ndani ishirini na matatu. Njia hiyo ya reli ni njia muhimu kuliko zote kwa nchi ya Zambia kufika pwani.

### Vocabulary

<b>reli</b>	railway, rails
<b>kuu</b>	great, big, important
<b>-unganisha</b>	merge, connect, link
<b>mipaka</b>	borders ( <i>sing.</i> <b>mpaka</b> )
<b>kati ya</b>	(in) between
<b>njia</b>	road
<b>-jengwa</b>	be built
<b>jamhuri</b>	republic
<b>ujenzi</b>	building construction, architecture
<b>daraja</b>	bridge(s)
<b>mashimo</b>	holes, pits, cavities ( <i>sing.</i> <b>shimo</b> )
<b>-penya</b>	penetrate ( <b>mashimo ya kupenya ndani</b> , tunnels <i>lit.</i> holes of penetrating inside)
<b>pwani</b>	coast

# 5 Safarini

## On the move

**In this unit you will learn:**

- how to make requests
- how to order food and drink
- how to give orders using the imperative form of the verb
- how to express wishes or desirable states using the optative form of the verb
- adjectives
- how to say you are hungry/thirsty/satisfied

### Dialogue 1

*Leo and Subira are in the dining-car, ordering their evening meal*

- 1 What type of fish is on the menu?
- 2 Leo asks for a food item that was not listed by the waiter. What is that food item?

MHUDUMU: Hamjambo?

LEO AND SUBIRA: Hatujambo.

MHUDUMU: Karibuni!

LEO AND SUBIRA: Asante!

MHUDUMU: Mnataka chakula gani?

SUBIRA: Sijaiona orodha ya vyakula. Kuna chakula gani?

MHUDUMU: Kuna wali na maharagwe, wali na kuku, wali na nyama, chipsi na kuku, chipsi na mayai, ugali na nyama.

LEO: Ndizi zipo?

MHUDUMU: Zipo.

LEO: Naomba ndizi na nyama.

SUBIRA: Kuna samaki?  
 MHUDUMU: Hakuna. Kuna nyama na kuku tu.  
 SUBIRA: Tafadhali nipe chipsi na kuku.  
 MHUDUMU: Nilete vinywaji?  
 LEO: Ndiyo. Kuna vinywaji gani?  
 MHUDUMU: Kuna chai, kahawa, soda, na pombe.  
 SUBIRA: Kuna soda gani?  
 MHUDUMU: Kuna 'coke', 'fanta', 'sprite' na tangawizi.  
 SUBIRA: Tafadhali lete coke.  
 LEO: Naomba chai ya rangi.

WAITER: *How are you?*  
 STUDENTS: *We are well.*  
 WAITER: *Welcome!*  
 STUDENTS: *Thanks!*  
 WAITER: *What food do you want?*  
 SUBIRA: *I haven't seen the menu. What sort of food is there?*  
 WAITER: *There's rice and beans, chicken and rice, meat and rice, chicken and chips, egg and chips, meat and 'ugali'.*  
 LEO: *Are there any bananas?*  
 WAITER: *Yes there are.*  
 LEO: *I'd like meat and bananas.*  
 SUBIRA: *Is there any fish?*  
 WAITER: *There isn't any. There's just meat and chicken.*  
 SUBIRA: *Please give me chicken and chips.*  
 WAITER: *Should I bring some drinks?*  
 VICTORIA: *Yes. What drinks are there?*  
 WAITER: *There's tea, coffee, soda and beer.*  
 SUBIRA: *What soft drinks do you have?*  
 WAITER: *There's coke, fanta, sprite and 'tangawizi'.*  
 SUBIRA: *Please bring a coke.*  
 LEO: *I would like a black tea.*

## Vocabulary

<b>mhudumu</b>	waiter, attendant
<b>chakula</b>	food ( <i>pl. vyakula</i> )
<b>-ona</b>	see
<b>orodha</b>	list, catalogue ( <b>orodha ya vyakula</b> , menu)
<b>wali</b>	cooked rice

<b>maharagwe</b>	beans ( <i>sing.</i> <b>haragwe</b> )
<b>kuku</b>	chicken(s)
<b>nyama</b>	meat
<b>ugali</b>	cooked maize meal
<b>ndizi</b>	banana(s) (savoury or sweet)
<b>-omba</b>	ask for, request, plea, pray for
<b>samaki</b>	fish(es)
<b>tafadhali</b>	please
<b>-leta</b>	bring
<b>vinywaji</b>	drinks, beverages
<b>chai</b>	tea ( <b>chai ya rangi</b> , <i>lit.</i> 'tea of colour', i.e. tea without milk)
<b>kahawa</b>	coffee
<b>pombe</b>	beer
<b>tangawizi</b>	ginger, ginger tea, ginger beer

## Language use

### ***Making orders and requests***

<b>-omba</b>	ask for, (beg, pray (for), appeal (to))
<b>-agiza</b>	order
<b>Naomba msaada</b>	I'd like some assistance
<b>Naomba radhi</b>	I beg forgiveness, I apologize
<b>Naagiza chakula</b>	I'd like some food
<b>Naagiza kinywaji</b>	I'd like a drink
<b>tafadhali</b>	please
<b>Tafadhali nipe kinywaji</b>	Please give me a drink
<b>Tafadhali lete chakula</b>	Please bring some food

### **Exercise 1**

Translate:

- 1 Je, unaomba msaada?
- 2 Msichana anaagiza kinywaji.
- 3 Sisi tunaomba orodha ya vyakula.
- 4 Je, mnaagiza vyakula gani?
- 5 Watalii wote wanaagiza chai.

## Exercise 2

Write these questions and requests in Swahili:

- 1 I would like a drink.
- 2 Please bring a soda.
- 3 We would like some tea.
- 4 Do you (*pl.*) want some fruit?
- 5 The tourist would like a pen (**kalamu**) and paper (**karatasi**).
- 6 Do you want a newspaper (**gazeti**)?

## Exercise 3

The verbs in column A are the opposites of those in B. Which verb in A is the opposite of the one in B?

A	B
-ondoka	-rudiana
-ingia	-chukua
-tengana	-simama
-kaa	-toka
-leta	-rudi
-kwenda	-fika

## Language structure

### ***Orders and the imperative form of the verb***

In Swahili orders are given by using the *imperative* form of the verb, which is the verb stem or, in the case of monosyllabic verbs, the verb plus stem marker:

<b>Soma!</b>	Read!
<b>Chukua!</b>	Take!
<b>Ondoka!</b>	Leave!
<b>Kumbuka!</b>	Remember!
<b>Sahau!</b>	Forget!
<b>Kula!</b>	Eat!
<b>Kunywa!</b>	Drink!

There are three irregular forms:

<b>Njoo!</b>	Come!	(from <b>kuja</b> )
<b>Nenda!</b>	Go!	(from <b>kwenda</b> )
<b>Lete!</b>	Bring!	(from <b>leta</b> )

When addressing many people, the *plural* form of the imperative is made by adding **-ni** (remember **Asanteni?**) to the singular form and changing final **-a** into **-e-**:

<b>Someni!</b>	Read!	
<b>Chukueni!</b>	Take!	
<b>Ondokeni!</b>	Leave!	
<b>Kumbukeni!</b>	Remember!	
<b>Sahauni!</b>	Forget!	
<b>Kuleni!</b>	Eat!	
<b>Kunyweni!</b>	Drink!	
<b>Njoooni!</b>	Come!	(often spelt <b>njoni</b> )
<b>Nendeni!</b>	Go!	
<b>Leteni!</b>	Bring!	

## Exercise 4

Translate into Swahili:

- 1 Come!
- 2 Go to school!
- 3 Drink some tea!
- 4 Order some coffee!
- 5 Eat!

## Language structure

### ***Wishes and the optative form of the verb***

The *optative* form of the verb is used to express wishes or desirable states. You form the optative by using the verb stem, changing the final **-a** to **-e**, and placing the appropriate participant marker or subject concord before it:

<i>Subject concord</i>	<i>Verbal base</i>	<i>Final</i>	
<b>ni</b>	<b>som</b>	<b>e</b>	that I may/should read
<b>wa</b>	<b>chuku</b>	<b>e</b>	that they may/should take
<b>ya</b>	<b>jengw</b>	<b>e</b>	that they ( <i>of a JI-MA class noun</i> ) may/should be built

Like other tenses, the optative can be used with the object concord:

<i>Subject concord</i>	<i>Object concord</i>	<i>Verbal base</i>	<i>Final</i>	
<b>a</b>	<b>mw</b>	<b>on</b>	<b>e</b>	that s/he may see him/her

In contrast to the imperative, monosyllabic verbs do not take the stem marker in the optative:

<i>Subject concord</i>	<i>Verbal base</i>	<i>Final</i>	
<b>ni</b>	<b>l</b>	<b>e</b>	so that I may/should eat
<b>a</b>	<b>l</b>	<b>e</b>	so that he may/should eat

The optative form is used very frequently, and may have a range of meanings as the examples below illustrate.

It is used for polite requests, rather than the imperative. In this use, the subject concord can be left out:

**Tafadhali usome orodha, or Tafadhali some orodha.**

Please read the list.

It is used for commands which involve an object marker:

<b>Umwite!</b> <i>or</i> <b>Mwite!</b>	Call him/her!
<b>Isome!</b>	Read it (e.g. <b>orodha</b> )!
<b>Nipe!</b>	Give me!

It is used to express intention or purpose:

**Alileta pasi tuichukue ubalozi.**

She brought her passport so that we could take it to the embassy.

**Walitupa viza tuingie.**

They gave us visas so that we could enter.

**Waite nisome nao.**

Call them so that I may study with them.

After some verbs of saying, e.g. **kuambia** (to tell), **kusema** (to say):

**Aliniambia nije.**

She told me to come.

**Je, walisema twende leo?**

Did they say we should go today?

After ‘modal’ words, expressing that something is better or necessary, such as the following:

**Afadhali twende kwa basi.**

It is better that we go by bus.

**Lazima waende nyumbani.**

They must go home.

**Heri niende sasa.**

I’d better go now.

**Inabidi tukate tiketi.**

We have to buy tickets.

The *negative optative* is formed by placing the negation marker **-si-** after the participant marker or subject concord:

<b>niende</b>	I should go	<b>nisiende</b>	I shouldn’t go
<b>uende</b>	you should go	<b>usiende</b>	you shouldn’t go
<b>mwende</b>	you ( <i>pl.</i> ) should go	<b>msiende</b>	you ( <i>pl.</i> ) shouldn’t go

**Usisahau** Don’t forget!

**Msikumbuke** Don’t remember (you all)!

**Exercise 5**

Replace the Swahili words written in the brackets with English.

The students who were without pens, [**mwalimu wao waliwaambia waende**] her office. Whilst in the office, the teacher searched inside her desk and later found some pens. Then [**aliwapa kalamu**]. The students took the pens and thanked her. She told them that [**lazima warudi darasani**] immediately as they had to finish their written test before the end of the class period. In the classroom one of the students told the teacher that her friend was too afraid to return



to the class because she was afraid of taking the written test. The teacher said, [**Mwite nimwone.**] When the girl returned to the class the teacher calmed her down and said, [**Afadhali ufanye**] the test today because the next test may be even more difficult.' The student wrote her test and passed.

## Exercise 6

Translate these sentences into English:

- 1 Nenda nyumbani. Mwite kaka yako. Mwambie aje hapa.
- 2 Njoooni shuleni kila siku. Msisahau.
- 3 Afadhali twende nyumbani.
- 4 Waambie wasiende. Lazima wakae hapa.
- 5 Usile mayai yangu! Kula yako!

## Dialogue 2

*Travelling on from Zimbabwe, the rest of the journey is completed on the road. After passing through Mozambique, the students have a short stay in Lilongwe, the capital of Malawi, then later they spend the last few remaining days resting by the lake at Nkata Bay. From there they take a bus to Karonga and then hitch a lift to the Malawi–Tanzania border. Leo and Victoria have already been questioned by an Immigration Official, now it's Subira and Trevor's turn*

- 1 What does Subira say she is doing in Tanzania?
- 2 How many countries in East Africa has Trevor been to?

OFISA UHAMIAJI: (After checking Subira's passport) Karibu tena Tanzania.

SUBIRA: Asante! Shikamoo!

OFISA UHAMIAJI: Marahaba! Je, unafanya nini hapa Tanzania?

SUBIRA: Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

OFISA UHAMIAJI: Kabla ya kurudi Tanzania, umekwenda wapi?

SUBIRA: Nimekwenda Zambia, Zimbabwe, Malawi na Msumbiji kabla ya kurudi hapa Tanzania.

OFISA UHAMIAJI: Habari za huko?

SUBIRA: Safi tu! Zambia ni nchi kubwa. Mji mkuu wa Zimbabwe, Harare, una majumba mapya mengi. Malawi ni nchi ndogo, lakini ina ziwa kubwa. Sijui habari za Msumbiji, tuliipita tu.

(Now Trevor is being asked some questions)

OFISA UHAMIAJI: Je, unajua Kiswahili?  
 TREVOR: Ndiyo bwana, ninajua Kiswahili.  
 OFISA UHAMIAJI: Karibu!  
 TREVOR: Asante!  
 OFISA UHAMIAJI: Je, unafanya nini hapa Tanzania?  
 TREVOR: Ninajifunza Kiswahili huko 'Mlimani'.  
 OFISA UHAMIAJI: Je, unasafiri peke yako?  
 TREVOR: La, ninasafiri pamoja na wanafunzi wenzangu.  
 OFISA UHAMIAJI: Habari za safari?  
 TREVOR: Njema. Sasa nimefika nchi tano za Afrika Mashariki; zote ni nzuri. Sasa ninataka kwenda nchi nyingine za Afrika Mashariki.

IMMIGRATION (After checking Subira's passport) *Welcome again to Tanzania.*  
 OFFICER:  
 SUBIRA: *Thanks! My respects!*  
 IO: *Respects welcome! What are you doing here in Tanzania?*  
 SUBIRA: *I'm a student at the University of Dar es Salaam.*  
 IO: *Prior to returning to Tanzania, where have you been?*  
 SUBIRA: *I've been to Zambia, Zimbabwe, Malawi and Mozambique, before coming back to Tanzania.*  
 IO: *What's it like over there?*  
 SUBIRA: *Just great! Zambia is a big country. The capital city of Zimbabwe, Harare, has many new buildings. Malawi is a small country, but it has a big lake. I really don't know anything about Mozambique, we just passed through it.*

(Now Trevor is being asked some questions)

IO: *Do you know Swahili?*  
 TREVOR: *Yes sir, I know Swahili.*  
 IO: *Welcome!*  
 TREVOR: *Thanks!*  
 IO: *What are you doing in Tanzania?*  
 TREVOR: *I'm studying Swahili over there at the University.*  
 IO: *Are you travelling by yourself?*  
 TREVOR: *No, I'm travelling with some student companions.*  
 IO: *How's the trip?*

TREVOR: *Good. Now I have gone to five East African countries, all are beautiful. Now I want to go to other countries in East Africa.*

## Vocabulary

<b>-kubwa</b>	( <i>adj.</i> ) big, large (important, elder, superior)
<b>mji mkuu</b>	capital city
<b>majumba</b>	buildings, mansions ( <i>sing.</i> <b>jumba</b> )
<b>mapya</b>	( <i>adj.</i> ) new ( <i>in reference to</i> <b>majumba</b> , buildings)
<b>mengi</b>	many ( <i>in reference to</i> <b>majumba</b> , buildings)
<b>ndogo</b>	( <i>adj.</i> ) little, small ( <i>in reference to</i> <b>nchi</b> , country)
<b>ziwa</b>	lake
<b>-pita</b>	pass (make a turn)
<b>-jifunza</b>	learn
<b>peke yako</b>	by yourself
<b>nyingine</b>	( <i>adj.</i> ) some, another ( <i>in reference to</i> <b>nchi nyingine za Afrika Mashariki</b> , other East African countries)

## Language point

**Mlimani** literally means ‘on the mountain/hill’. The University of Dar es Salaam is situated on Observation Hill outside the city centre, thus ‘**Mlimani**’ is a nickname for the university.

## Language structure

### Adjectives

Like possessives and numbers, adjectives agree with the noun they refer to. In general, the adjective concord is the same as the nominal prefix which is found at the beginning of the word to show which class it belongs to. Adjectives usually express a quality or state of the noun they modify. Some adjective stems are given below:

<b>-kubwa</b>	big	<b>-dogo</b>	small
<b>-pana</b>	wide	<b>-embamba</b>	narrow, thin
<b>-refu</b>	tall, long	<b>-fupi</b>	short

<b>-zuri</b>	good, pretty	<b>-baya</b>	bad, ugly
<b>-pya</b>	new	<b>-gumu</b>	hard, difficult
<b>-kuu</b>	big, important		

These adjectival stems are used with nouns from the noun classes discussed so far as shown below:

#### M-WA

<b>mtu mkubwa</b> a big man	<b>watu wakubwa</b> big people
<b>Mzambia mzuri</b> a beautiful Zambian	<b>Wazambia wazuri</b> beautiful Zambians

#### N

<b>treni kubwa</b> a big train	<b>treni kubwa</b> big trains
<b>habari fupi</b> a short news item	<b>habari fupi</b> short news

*But note:*

<b>rafiki mfupi</b> a short friend	<b>rafiki wafupi</b> short friends
---------------------------------------	---------------------------------------

#### JI-MA

<b>behewa kubwa</b> a big carriage	<b>mabehewa makubwa</b> big carriages
<b>jina zuri</b> a beautiful name	<b>majina mazuri</b> beautiful names

As a general rule, the adjective stem takes a prefix whenever the noun takes a prefix, as for example in the M-WA class and the plural of the JI-MA class. On the other hand, there is no adjective agreement with those nouns which do not have a prefix: the N class and the singular of the JI-MA class.

Some exceptions to this pattern are found with (1) vowel initial stems, (2) the monosyllabic adjective stem **-pya**, and (3) with some adjective stems in the N class. Most exceptions are very similar to those also found with nouns.

## Vowel initial stems

The first important exception concerns adjective stems beginning with a vowel. The most important of these stems are given below:

<b>-ingine</b>	other, different	<b>-ekundu</b>	red
<b>-ingi</b>	many	<b>-eupe</b>	white
<b>-ema</b>	good, well	<b>-eusi</b>	black
<b>-embamba</b>	narrow, thin		

The prefix changes due to the following vowel:

M-WA

<b>mtu mwingine</b>	<b>watu wengine</b>
a different man	other people
<b>Mzambia mwembamba</b>	<b>Wazambia wembamba</b>
a thin Zambian	thin Zambians

N

<b>treni nyingine</b>	<b>treni nyingine</b>
a different train	different trains
<b>treni nyekundu</b> a red train	<b>treni nyekundu</b> red trains

*But:*

<b>habari njema</b>	<b>habari njema</b>
a good news item	good news

JI-MA

<b>behewa jingine</b>	<b>mabehewa mengine</b>
a different carriage	different carriages
<b>jina jema</b>	<b>majina mema</b>
a good name	good names

The rules are that **m-** becomes **mw-**, **wa-** combines with **-i** or **-e** to form **we-**, N-class nouns take **ny-**, and JI-MA nouns take **j-** in the singular (sometimes **l-** is heard instead of **j-**), and have **me-** in the plural. Note the exception of **-ema** with N-class nouns: it is **njema**.

## The stem -pya

The second exception is found with monosyllabic adjective stems. In classes where adjective stems do not normally take a prefix,

some short (monosyllabic) stems do. Of the stems we have here, this exception affects only **-pya**, ‘new’ when agreeing with a singular JI-MA noun or with an N-class noun:

<b>Jino jipya</b>	a new tooth
<b>Safari mpya</b>	a new journey/new journeys

As can be seen from the examples, **-pya** takes a **ji-** prefix with JI-MA singular nouns, and an **m-** prefix in the N class.

## Adjective stems in the N class

The third exception concerns only adjectives agreeing with N-class nouns. In the N class, stems beginning in **d**, **g**, **z**, or **r** take, in contrast to other stems, an **n-** prefix:

<b>safari ndogo</b>	a small journey
<b>safari nzuri</b>	a beautiful journey
<b>safari ngumu</b>	a hard, difficult journey
<b>safari ndefu</b>	a long journey ( <i>from -refu: -r- changes to -d-</i> )

With all other stems, there is no adjective agreement in the N class (except, of course, for vowel initial stems and **mpya**).

A number of adjectives, mostly those which have entered the Swahili language more recently, do not agree with their head noun. For example, **buluu**, ‘blue’, **muhimu**, ‘important’, or **maalum**, ‘special’, are used with any noun without changes:

<b>behewa buluu</b>	blue carriage
<b>mtu muhimu</b>	important person
<b>mwalimu buluu</b>	blue teacher
<b>treni maalum</b>	special train

## Exercise 7

Replace the adjective written in English in the passage below with the appropriate Swahili equivalent:

Wanafunzi *four* wanakwenda Zambia kwa treni. Treni hii ni *big* yenye mabehewa *many*. Rangi ya treni hiyo ni *red* na *white*. Ni safari *long*. Katika treni, Mzambia *tall* na mke wake *short* wanazungumza na wanafunzi. Wanafunzi wanapata habari *important* kuhusu nchi ya Zambia.

## Exercise 8

Match the nouns in column A with the appropriate adjective in column B:

A	B
safari	weusi
jina	mweupe
mtu	jipya
mabehewa	ndefu
watu	nzuri
habari	mengi

## Dialogue 3

*Travelling on from the border, the bus to Dar es Salaam stops periodically at stations and refreshment centres. It is at these places where local people, mainly women and children, sell snacks and light refreshment to the bus travellers*

- 1 What food items do the students buy?
- 2 How much does each item cost?
- 3 What does Subira do with the items she bought?

MWUZAJI WA 1: Maandazi! Maandazi!

MWUZAJI WA 2: Machungwa matamu hapa! Machungwa matamu hapa!

MWUZAJI WA 1: Soda baridi! Soda baridi!

MWUZAJI WA 2: Mifuko ya miwa! Mifuko ya miwa!

VICTORIA: Naona njaa. Maandazi ni shilingi ngapi?

MWUZAJI WA 1: Shilingi mia moja.

VICTORIA: Naomba manne. Chukua pesa hizi, shilingi mia nne.

MWUZAJI WA 1: Asante!

VICTORIA: Je, machungwa haya ni matamu kweli?

MWUZAJI WA 2: Ndiyo, ni matamu sana. Onja hili.

VICTORIA: Mmm, ni tamu. Nipe sita basi. Bei gani?

MWUZAJI WA 2: Sita ni shilingi mia tatu.

LEO: Naona kiu. Kijana! Lete soda hapa!

MWUZAJI WA 1: Unataka soda ngapi?

LEO: Nataka nne. Baridi sana.

MWUZAJI WA 1: Chukua hizi, zote baridi. Ni shilingi mia nane kwa jumla.

LEO: Haya, shukrani.  
Je, mfuko mmoja wa miwa ni bei gani?

MWUZAJI WA 2: Shilingi mia moja tu.

LEO: Haya, lete moja. Asante!  
Subira, Trevor na Victoria chukueni soda.

SUBIRA, TREVOR

AND VICTORIA: Asante!



SELLER 1: *Doughnuts! Doughnuts!*

SELLER 2: *Sweet oranges here! Sweet oranges here!*

SELLER 1: *Cold drinks! Cold drinks!*

SELLER 2: *Bags of sugarcane! Bags of sugarcane!*

VICTORIA: *I feel hungry. How much are the doughnuts?*

SELLER 1: *A hundred shillings.*

VICTORIA: *I want four. Take this money, four hundred shillings.*

SELLER 1: *Thanks!*

VICTORIA: *Are these oranges really sweet?*

SELLER 2: *Yes, they are very sweet. Taste this one.*

VICTORIA: *Mmm, it is sweet. Well then, give me six. What's the price?*



- SELLER 2: *Six is three hundred shillings.*  
 LEO: *I feel thirsty. Hey youth! Bring some soft drinks here!*
- SELLER 1: *How many drinks do you want?*  
 LEO: *I want four. Very cold (ones).*  
 SELLER 1: *Take these, all are cold. They are eight hundred shillings all together.*
- LEO: *OK, thanks. What price is one bag of sugarcane?*  
 SELLER 2: *Only one hundred shillings.*  
 LEO: *OK, bring one. Thanks! Subira, Trevor and Victoria, take a soda.*
- SUBIRA, TREVOR  
 AND VICTORIA: *Thanks!*

## Vocabulary

<b>maandazi</b>	doughnuts, pastries ( <i>sing. andazi</i> )
<b>baridi</b>	( <i>adj.</i> ) cold, cool (mild)
<b>mifuko</b>	bags, sacks (pockets, purses; <i>sing. mfuko</i> )
<b>njaa</b>	hunger (famine, starvation, <b>Naona njaa</b> , I feel hungry)
<b>-onja</b>	taste
<b>kiu</b>	thirst
<b>kijana</b>	youth ( <i>pl. vijana</i> )
<b>shukrani</b>	thanks, gratitude

## Language use

### *You feel hungry/thirsty/satisfied*

<b>-ona</b>	see, feel
<b>-sikia</b>	hear, feel
<b>Ninaona njaa,</b> <b>Ninasikia njaa</b> <b>Nina njaa</b>	I feel hungry, I'm hungry
<b>Naona kiu, ninasikia kiu</b>	I feel thirsty, I'm thirsty
<b>Nimeshiba</b>	I'm satisfied, I've had enough food/drink, I'm full

## Exercise 9

You have just entered a shop and you want to buy some goods. Here is a conversation that takes place between yourself and a shopkeeper. Answer by changing the English in the brackets into Swahili:

MWUZAJI: Karibu!

MIMI: Asante! [*I want some oranges and bananas.*]

MWUZAJI: Unataka machungwa mangapi na ndizi ngapi?

MIMI: Nataka [*twelve oranges and twelve bananas*].

MWUZAJI: Je, unataka vitu vingine?

MIMI: [*Yes*], nataka maji ya kunywa, soda, [*tea and coffee*].

MWUZAJI: [*What sort of soda do you want?*]

MIMI: [*Please give me one fanta and two sprite. How much is it?*]

MWUZAJI: [*The price is*] shilingi elfu moja na mia tisa [*in total*].

MIMI: [*Take this money.*] Asante!

MWUZAJI: [*OK*] Karibu tena. [*Goodbye!*]

MIMI: Kwaheri!

## Reading

### Jiografia ya Tanzania

Tanzania ni nchi kubwa; iko Afrika Mashariki. Nchi hiyo ipo kusini kidogo tu ya Mstari wa Ikweta. Katika mashariki ya nchi hiyo ipo Bahari ya Hindi. Nchi zilizo jirani na Tanzania ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (iliyoitwa Zaire), Zambia, Malawi na Msumbiji. Visiwa vya pwani ni Unguja na Pemba (Zanzibar). Kuna maeneo muhimu mawili ya jiografia ndani ya nchi ya Tanzania. Moja ni Mlima Kilimanjaro ambao ni mlima mrefu kuliko yote iliyomo Afrika. Mlima Kilimanjaro ni mnara wa Afrika na urefu wake toka usawa wa bahari ni futi 19,340. Eneo jingine muhimu ni lile Bonde la Ufa linalopita sehemu nyingi za Afrika Mashariki hadi Asia.

### Vocabulary

<b>mashariki</b>	east
<b>kusini</b>	south
<b>mstari</b>	line

<b>Bahari ya Hindi</b>	the Indian Ocean
<b>jirani</b>	neighbour
<b>pwani</b>	coast
<b>maeneo</b>	regions, areas
<b>mnara</b>	tower
<b>Bonde la Ufa</b>	the Rift Valley

# 6 Shambani

## In the countryside

**In this unit you will learn:**

- the demonstratives 'this', 'that', 'these' and 'those'
- more about numbers
- how to make comparisons

### Dialogue 1

*Amos has decided to go and visit his family who live in Bukoba, Lake Victoria, close to the Tanzania-Uganda border. The American student Kathy has expressed her interest to see as much of Tanzania as possible, and so he has invited her to accompany him on this trip. After a very long journey (more than 40 hours!), Amos is now introducing his family to Kathy*

1 Mzee Kiaruzi has a preference. What is it?

2 Kathy has a preference. What is it?

AMOS: Huyu ni babangu, Mzee Kiaruzi.

KATHY: Shikamoo Mzee!

M. KIARUZI: Marahaba! Karibu sana.

KATHY: Asante.

AMOS: Huyu ni mamangu, Bibi Zakia.

KATHY: Shikamoo mama!

BI. ZAKIA: Marahaba! Karibu kwetu.


KATHY: Asante sana.

M. KIARUZI: *(To Amos)* Jamani! Mgeni huyu anajua Kiswahili.

AMOS: Ndiyo, anajua sana. Yeye anajifunza Kiswahili chuo kikuu.

M. KIARUZI: *(To Kathy)* Karibu shambani.

- KATHY: Asante. Ni pazuri hapa.  
 M. KIARUZI: Ndiyo. Hapa ni mazingira ya kupendeza. Pana mandhari nzuri yenye milima, mito na maziwa. Tofauti kabisa na mandhari ile ya miji yenye magari na mavumbi. Mimi napenda maisha ya shambani kuliko maisha ya mjini. Je, umewahi kuliona Ziwa Victoria?  
 KATHY: Kwa mbali tu.  
 M. KIARUZI: Jioni mke wangu atakupikia samaki wanaotoka katika ziwa hilo. Bila shaka utawapenda.  
 BI. ZAKIA: Je, unapenda ndizi?  
 KATHY: Ndiyo, nazipenda kuliko wali.  
 BI. ZAKIA: Kuna migomba mingi hapa Bukoba, kwa hiyo watu wa hapa wanakula ndizi karibu kila siku. Basi nitapika ndizi vilevile.



- AMOS: *This is my father, Elder Kiaruzi.*  
 KATHY: *My respects Elder!*  
 M. KIARUZI: *Respects taken! You are most welcome!*  
 KATHY: *Thanks.*  
 AMOS: *This is my mother, Mrs Zakia.*  
 KATHY: *My respects mother!*  
 BI. ZAKIA: *Respects taken! You are welcome to our home.*  
 KATHY: *Many thanks.*  
 M. KIARUZI: (To Amos) *My goodness! This foreigner knows Swahili.*  
 AMOS: *Yes, she knows a lot. She is studying Swahili at the university.*

- M. KIARUZI: (To Kathy) *Welcome to the countryside.*  
 KATHY: *Thanks. It's beautiful here.*  
 M. KIARUZI: *Indeed. This place is a nice environment. There's beautiful scenery with mountains, rivers and lakes. Entirely different from the scenery of the towns with their vehicles and dust. I like life in the countryside more than life in town. Have you managed to see Lake Victoria?*  
 KATHY: *Only from a distance.*  
 M. KIARUZI: *In the evening my wife will cook some fish for you which come from that lake. No doubt you will like them.*  
 BI. ZAKIA: *Do you like bananas?*  
 KATHY: *Yes, I prefer them to cooked rice.*  
 BI. ZAKIA: *There are many banana plants here in Bukoba, so people from here eat bananas nearly every day. Well then, I shall also cook some bananas.*

## Vocabulary

<b>kwetu</b>	at our place, at us
<b>mgeni</b>	visitor, guest, foreigner, stranger, new person
<b>-jua</b>	know
<b>pazuri</b>	nice, fine, beautiful ( <b>pa</b> + <b>zuri</b> in reference to a place)
<b>mazingira</b>	environment
<b>-a kupendeza</b>	pleasing, charming, attractive
<b>pana</b>	there is
<b>mandhari</b>	scenery
<b>yenye</b>	having, with (in reference to <b>mandhari</b> )
<b>milima</b>	mountains (sing. <b>mlima</b> )
<b>mito</b>	rivers (sing. <b>mto</b> )
<b>maziwa</b>	lakes, ponds (sing. <b>ziwa</b> )
<b>magari</b>	cars, vehicles (sing. <b>gari</b> )
<b>mavumbi</b>	dust (sing. <b>vumbi</b> )
<b>-wahi</b>	manage, reach, be on time for
<b>kwa mbali</b>	from a distance, afar
<b>-pikia</b>	cook for (from <b>-pika</b> , cook)
<b>samaki</b>	fish
<b>-penda</b>	like, love
<b>ndizi</b>	bananas
<b>kuliko</b>	than (in comparison)
<b>migomba</b>	banana plants (sing. <b>mgomba</b> )
<b>karibu</b>	near, nearby, nearly

## Language structure

### ***Demonstratives: 'this', 'that', 'these' and 'those'***

There are three kinds of demonstratives in Swahili, two of which point to something near and far, and a third kind for something which has already been mentioned, or been 'referred to', and is thus known to the speaker and the person who is spoken to.

We have already seen demonstratives in previous units and there are a number of demonstratives in Dialogue 1 of this unit. For example, the Dialogue opens with Amos saying: ***Huyu ni babangu ... Huyu ni mamangu ...*** 'This (person) is my father ...' 'This (person) is my mother ...'. Later Amos's father, Mzee Kiaruzi says: ***Mgeni huyu anajua Kiswahili.*** 'This guest/foreigner knows Swahili.' These are instances of a demonstrative referring to a person (an M-WA noun) near the speaker.

Later on in the dialogue Mzee Kiaruzi says to Kathy: ***Jioni mke wangu atakupikia samaki wanaotoka katika ziwa hilo.*** 'In the evening my wife will cook some fish for you which comes from that lake (already referred to).' Because he has already mentioned Lake Victoria, Kathy knows what he is referring to. Later, Mzee Kiaruzi uses the demonstrative 'that' when he says: ***Tofauti kabisa na mandhari ile ya miji.*** 'Completely different from that town environment.'

In Swahili the demonstrative must agree with the noun it qualifies. All three types of demonstrative are formed with the concord, as can already be seen from the examples in the text – ***huyu*** includes the M-WA singular marker ***yu-***, while the ***i-*** in ***ile*** and the ***-lo*** in ***hilo*** are formed from the N-class and the JI-MA class singular concords.

### ***Demonstratives showing 'nearness': 'this', 'these'***

All begin with ***h-*** and end with the appropriate concord. Between the two, the same vowel present in the concord is repeated. Thus in the above examples we get ***huyu*** for 'this (person)'.  
 All begin with ***h-*** and end with the appropriate concord. Between the two, the same vowel present in the concord is repeated. Thus in the above examples we get ***huyu*** for 'this (person)'.

### ***Demonstratives showing ‘farness’: ‘that’, ‘those’***

All begin with the concord and end with **-le**. So, the above example **mandhari ile**, ‘that scenery’, is made up of the N-class singular concord **i** and the demonstrative marker for ‘farness’ **le**, **i + le = ile** ‘that’.

### ***Demonstratives of reference: ‘that’, ‘those (referred to)’***

All begin with **h-** and end with **-o**, as in the above example . . . **ziwa hilo**, ‘. . . that lake (referred to)’.

The following table shows the three demonstratives for the three classes we have introduced so far:

<i>Singular</i>	<i>Plural</i>
<b>M-WA Class</b>	
<b>mtu huyu</b> this person	<b>watu hawa</b> these people
<b>mtu yule</b> that person	<b>watu wale</b> those people
<b>mtu huyo</b> that person (referred to)	<b>watu hao</b> those people (referred to)
<b>JI-MA Class</b>	
<b>tunda hili</b> this fruit	<b>matunda haya</b> these fruits
<b>tunda lile</b> that fruit	<b>matunda yale</b> those fruits
<b>tunda hilo</b> that fruit (referred to)	<b>matunda hayo</b> those fruits (referred to)
<b>N Class</b>	
<b>nyumba hii</b> this house	<b>nyumba hizi</b> these houses
<b>nyumba ile</b> that house	<b>nyumba zile</b> those houses
<b>nyumba hiyo</b> that house (referred to)	<b>nyumba hizo</b> those houses (referred to)



## Reduplication

Any of the demonstratives outlined above may be repeated. This then intensifies the meaning, e.g.

<b>mtu huyu huyu</b>	this very same person
<b>mtu yule yule</b>	that very same person
<b>mtu huyo huyo</b>	that same person (mentioned)

## Exercise 1

Write the Swahili equivalent of the word in brackets:

E.g. **Mtu** (*that*) **yule** **Watu** (*these*) **hawa**

- |                                                    |                                        |
|----------------------------------------------------|----------------------------------------|
| 1 mtu ( <i>this</i> )                              | 6 nyumba ( <i>this</i> )               |
| 2 watu ( <i>those</i> )                            | 7 nyumba ( <i>these</i> )              |
| 3 mgeni ( <i>referred to</i> )                     | 8 mtu ( <i>this very same person</i> ) |
| 4 tunda ( <i>referred to</i> )                     | 9 matunda ( <i>those</i> )             |
| 5 watu ( <i>those very same people mentioned</i> ) |                                        |

## Exercise 2

Fill in the gaps then translate the sentences into English:

E.g. **Mtoto huyu ni wangu.** This child is mine.

- 1 Nyumba i . . . ni nzuri.
- 2 Nyumba z . . . si nzuri.
- 3 Wageni h . . . wanajua Kiswahili.
- 4 Wageni h .o hawajui Kiswahili.
- 5 Mmarekani y . . . anaondoka leo.
- 6 Mwingereza h . . . ataondoka kesho.

## Dialogue 2

*The following day, Amos takes Kathy for some sightseeing close to the lake*

KATHY: Jamani! Ziwa Victoria ni kubwa mno kama bahari.

AMOS: Ndiyo. Watu wengi wanapata riziki zao kutokana na ziwa hilo. Kuna mabaharia, wavuvi na wasaidizi wao. Watu

wengine wanafanya kazi si mbali na hapa, pale mashambani. Watu hao wanalima kahawa, pamba, matunda na mboga. Katika shamba letu tumepanda miti mingi. Vilevile tunalima mboga za aina mbalimbali.

KATHY: Je, shamba lenu lina miti mingapi?

AMOS: Lina michungwa kumi na miwili, milimao kumi, miembe minane, michikichi sita, minazi mitano na mfenesi mmoja tu.

KATHY: Hakuna migomba?

AMOS: Kuna migomba mingi na mimea mingine, lakini sijui mingapi hasa. Je, unataka kwenda shambani?

KATHY: Ndiyo, twende!

KATHY: *My goodness! Lake Victoria is vast like the sea.*

AMOS: *Yes. Many people get their daily needs from the lake (lit. as a result of the lake). There are sailors, fishermen and their helpers. Other people work not far from here in the fields. These people cultivate coffee, cotton, fruit and vegetables. In our field we've planted many trees. We are also cultivating various kinds of vegetables.*

KATHY: *How many trees does your field have?*

AMOS: *It has twelve orange trees, ten lemon trees, eight mango trees, six palm oil trees, five coconut palms and just one jackfruit tree.*

KATHY: *There are no banana plants?*

AMOS: *There are many banana plants and other crops, but I don't know how many exactly. Do you want to go to the field?*

KATHY: *Yes, let's go!*

## Vocabulary

<b>mno</b>	much too much, to excess
<b>bahari</b>	sea, ocean
<b>riziki</b>	daily needs, God's blessings
<b>kutokana na</b>	as a result of
<b>mabaharia</b>	sailors ( <i>sing. baharia</i> )
<b>wavuvi</b>	fishermen ( <i>sing. mvuvi</i> )
<b>wasaidizi</b>	assistants, helpers ( <i>sing. msaidizi</i> )
<b>mashamba</b>	fields ( <i>sing. shamba, also means</i> the countryside)
<b>-lima</b>	cultivate
<b>pamba</b>	cotton, cotton wool

<b>mboga</b>	vegetable(s) ( <i>also</i> some meat as a side dish, <i>or</i> a pushover, someone who is easy to fool)
<b>-panda</b>	plant, sow

## Language structure

### *The M-MI noun class*

A number of words in the dialogue belong to a new noun class (the fourth discussed so far), the M-MI class.

<i>Singular</i>	<i>Plural</i>	
<b>mti</b>	<b>miti</b>	tree
<b>mchungwa</b>	<b>michungwa</b>	orange tree
<b>mnazi</b>	<b>minazi</b>	coconut palm
<b>mgomba</b>	<b>migomba</b>	banana plant

This class is sometimes called the ‘tree class’, but a number of other nouns belong here as well:

<b>mlima</b>	<b>milima</b>	mountain, hill
<b>mto</b>	<b>mito</b>	river
<b>mji</b>	<b>miji</b>	town

When followed by a vowel, singular nouns begin with **mw-**:

<b>mwembe</b>	<b>miembe</b>	mango tree
<b>mwaka</b>	<b>miaka</b>	year
<b>mwezi</b>	<b>miezi</b>	month, moon

The M-MI class has the following agreement:

	<i>Concord</i>	<i>Possessive concord</i>	<i>Adjective concord</i>	<i>Demonstratives</i>
<i>Sing.</i>	<b>u-</b>	<b>w-</b>	<b>m-</b>	<b>huu ule huo</b>
<i>Pl.</i>	<b>i-</b>	<b>y-</b>	<b>mi-</b>	<b>hii ile hiyo</b>

**Mti wangu huu unapendeza.**

This tree of mine pleases.

**Miti yako mizuri inapendeza.**

Your beautiful trees please.

## Language structure

In Swahili the numbers 1, 2, 3, 4, 5, and 8 are treated just like other adjectives, that is, they agree with the noun they qualify. In general counting, the numbers of the N class are used (as already introduced in Units 3, 4, and 5):

1	<b>-moja</b>	11	<b>kumi na -moja</b>
2	<b>mbili (-wili)</b>	12	<b>kumi na mbili (-wili)</b>
3	<b>-tatu</b>	13	<b>kumi na -tatu</b>
4	<b>-nne</b>	14	<b>kumi na -nne</b>
5	<b>-tano</b>	15	<b>kumi na -tano</b>
6	<b>sita</b>	16	<b>kumi na sita</b>
7	<b>saba</b>	17	<b>kumi na saba</b>
8	<b>-nane</b>	18	<b>kumi na -nane</b>
9	<b>tisa</b>	19	<b>kumi na tisa</b>
10	<b>kumi</b>	20	<b>ishirini</b>

In the case of **mbili** (2) this changes to **-wili** when the noun is not of the N class. For example, in Dialogue 2 Amos tells Kathy that the family plot has *michungwa kumi na miwili*, ‘twelve orange trees’. **Mi-** is the marker for a plural noun of the M-MI class (the singular is **m-**), and so with the pattern of agreement **-wili** takes the **mi-** prefix. The chart shows how this works in the classes introduced so far:

<i>Noun</i>	1	2	3	4	5	8
<b>mtu</b>	mmoja					
<b>watu</b>		wawili	watatu	wanne	watano	wanane
<b>mti</b>	mmoja					
<b>miti</b>		miwili	mitatu	minne	mitano	minane
<b>nen</b>	moja					
<b>maneno</b>		mawili	matatu	manne	matano	manane
<b>nyumba</b>	moja					
<b>nyumba</b>		mbili	tatu	nne	tano	nane

This is a good time to mention word order. In Swahili the noun is followed by the adjective, then the number and, lastly, the demonstrative (generally this is the opposite of the word order in English, but this is liable to change with emphasis). For example:

**Watoto wadogo wanne hawa**

These four small children

(*lit.* Children small four these)

**Minazi mikubwa kumi na mmoja hii**

These eleven big coconut palms

(*lit.* Coconut palms big ten and one these)

### Exercise 3

Translate these sentences into English.

E.g. **Watoto kumi na wawili hawa** These twelve children

- 1 Mtoto mmoja ni wangu na mtoto mmoja ni wake.
- 2 Watu wawili wale wanatoka Dar es Salaam.
- 3 Miti mitatu hii ni yangu na miti kumi na miwili ile ni yako.
- 4 Soma majina matano haya.
- 5 Nyumba sita hizi ni mpya.
- 6 Watu saba hawa walifika jana.
- 7 Watoto wanane hao wako shuleni.
- MAMA: Na mama yule anayecheza ngoma za chakacha na lele-mama, si mwanamke yuleyule apendaye kupika chakula?
- BIARUSI: Ndiyo, ni yuleyule. Ndiye mtu apikaye chakula kwa watu wafanyao kazi mlimani. Baba huenda kwenye kibanda chake kwa chakula cha mchana.
- MAMA: Bila shaka chakula apikacho ni kitamu sana. Je, unakubali?
- BIARUSI: Nakubali. Vyote atengenezavyo ni vizuri kupita kiasi. Kweli mwanamke huyu pamoja na mwimbaji huyo, na jamaa zetu, wamefanya arusi yetu iwe siku ya kukumbukwa.

## Vocabulary

<b>aliye</b>	s/he who is ( <i>see Language structure below</i> )
<b>apendaye</b>	who likes ( <i>see Language structure below</i> )
<b>-kuta</b>	find, meet
<b>lichya ya</b>	besides, aside from, let alone, despite
<b>-amua</b>	decide
<b>ngoma</b>	traditional dance(s), drum(s) ( <i>The <b>chakacha</b> and <b>lelemama</b> are traditional dances performed by women at weddings.</i> )
<b>kibanda</b>	shed, hut, kiosk
<b>-kubali</b>	agree (permit, accept)
<b>atengenezavyo</b>	which s/he prepares
<b>kupita kiasi</b>	better/more than usual, <i>lit.</i> to surpass the average amount
<b>-kumbukwa</b>	be remembered

## Language structure

### *The general relative*

The final relative strategy is the general relative. This construction is not as frequent as the other two strategies, but you will encounter it especially in writing. In the general relative, the referential concord is placed immediately after the verbal base, which is preceded by the subject (and possibly object) concord. There is no tense marker in the general relative:

**Mtu apendaye kahawa.**

The person who likes coffee.

**Watu wapikao chakula.**

The people who cook the food.

The general relative combined with the special verb **-li-**, ‘be’, can be used to form relatives of the copula (this **-li-** is not the past tense marker **-li-**):

<b>mimi niliye</b>	I who/am
<b>wao walio wageni</b>	they who are strangers
<b>mambo yaliyomo</b>	the things which are inside
<b>vyombo vilivyopo mezani</b>	the utensils which are on the table

**Exercise 6**

Can you spot the words which have been written with the wrong referential concord in the passage below?

Arusi ya Bw Yusufu na Bi Subira ilikuwa sherehe nzuri sana. Watu wote ambacho walikuwapo walicheza densi na walikula chakula kitamu kililopikwa na mpishi aliotoka Tanga. Baada ya sherehe, Bw. na Bi Arusi walisafiri Moshi ambaye watapanda Mlima Kilimanjaro.

**Reading****Ndoa**

Mitazamo ya watu kuhusu mambo ya ndoa inatofautiana. Tofauti hizo zinatokana na jinsia, umri, au desturi za watu wanaohusika. Data inayotokana na takwimu za siku hizi zinaonyesha tofauti za mtazamo kati ya wanaume na wanawake, watu wa miaka ya 1960 na wa siku hizi, na pia kati ya nchi tatu za Afrika ya Mashariki, yaani Tanzania, Kenya, na Uganda.

Kwa mfano, wanawake wanaolewa wakiwa na umri mdogo zaidi kuliko wanaume. Nchini Tanzania, asilimia 70 ya wanawake ambao wana umri baina ya miaka 20–24 wameshaolewa, ambapo asilimia 30 tu ya wanaume wa rika hilohilo wameoa. Walakini, katika rika la miaka 35–39, hakuna tofauti baina ya wanawake na wanaume, kwa maana zaidi ya asilimia 80 ya wote wawili, wanawake na wanaume wameoana.

Katika miaka thelathini iliyopita wanawake na wanaume wengi waliamua kuoa wakiwa na umri mkubwa zaidi. Kwa mfano, nchini Kenya, katika mwaka 1969 asilimia 26 ya wanaume, na asilimia 76 ya wanawake wameolewa kabla hawajafikia umri wa miaka 25. Katika mwaka 1998, takwimu hizo zimebadilika kuwa asilimia 16 ya wanaume na asilimia 58 ya wanawake ambao wameolewa.

Zaidi ya asilimia 10 ya wanawake wa Tanzania wenye umri zaidi ya miaka 50 ni watalaka au wametengana na waume zao. Kwa upande mwingine, karibu asilimia 7 tu ya wanaume wa Tanzania ni watalaka. Katika nchi ya jirani, Kenya, idadi ya watu ambao wametengana au walio watalaka wenye umri zaidi ya miaka 50 inapungua zaidi kuwa asilimia 3 kwa jinsia zote mbili. Nchini Uganda, idadi ya watu ambao wametengana au walio watalaka ndiyo kubwa zaidi kuliko zote katika Afrika Mashariki, kuwa asilimia 20 kwa jinsia zote mbili zenye umri zaidi ya miaka 50.

## Vocabulary

<b>mitazamo</b>	viewpoints, attitudes ( <i>sing. mtazamo</i> )
<b>-tofautiana</b>	be different
<b>tofauti</b>	difference
<b>-tokana na</b>	result/stem from
<b>jinsia</b>	gender, sex
<b>desturi</b>	custom(s), way(s)
<b>-husika</b>	be involved, be concerned, be applicable
<b>takwimu</b>	statistic(s)
<b>kwa mfano</b>	for example ( <i>abbreviated k.m.</i> )
<b>asilimia</b>	per cent
<b>hali</b>	while, seeing that, when
<b>rika</b>	age group, contemporary, peer
<b>walakini</b>	but, however
<b>kwa maana</b>	because, since, that is to say
<b>-badilika</b>	be changed
<b>kwa upande mwingine</b>	on the other hand (from the other direction)
<b>karibu</b>	nearly (near, nearby)
<b>jirani</b>	neighbour
<b>idadi</b>	total, number (population)
<b>walio</b>	they who are ( <b>wa + li + o</b> )
<b>-pungua</b>	diminish, decrease, be reduced

# 11 Taabu za nyumbani

## Trouble at home

### In this unit you will learn:

- the situational tense **-ki-**
- the conditional tenses **-nge-** and **-ngali-**
- the reciprocal extension **-an-**
- how to bring your point across
- how to reason hypothetically
- how to use words to structure arguments

## Dialogue 1

*Tatu and her brother, Hadji, are quarrelling. The dispute is about the various ways to cook rice*

- 1 According to Tatu, how does her mother cook rice?
- 2 According to Hadji, how does his mother cook rice?
- 3 What does the mother say about her own cooking methods?

TATU: Ukiukoroga wali wakati unapochemka utagandana.

HADJI: Nabisha! Usipoukoroga wali utakuwa kama mchanga.

TATU: Sivyoy! Nabisha! Ukimwona mama anapika wali utaona kwamba yeye haukorogi wali. Mama atauacha uchemke polepole hadi maji yametoweka.

HADJI: Ulikuwa wapi wewe mama yetu alipopika wali? Au ulikuwa kipofu? Mama hukoroga wali wakati unapopikwa.

*(Mother enters the kitchen)*

MAMA: Kuna nini hapa? Mbona mnabishana nyinyi? Mbona mnapiga kelele?

- TATU: Hadji anasema kwamba wewe hukoroga wali wakati unapopikwa, na mimi nasema sivyo hivyo.
- MAMA: Jinsi hizo zote mbili ni sawa. Inategemea aina ya mchele ambao nitautumia. Baadhi ya michele inahitaji kukoroga na mingine inahitaji iachwe. Kwa hiyo nyinyi nyote mnasema ukweli.
- HADJI: Tatu inaonekana kwamba mabishano yetu yalikuwa kazi bure.
- TATU: Ndiyo. Sasa tunajua kwamba kuna jinsi kadha za kupika wali. Tafadhali mama tufundishe.

## Vocabulary

-koroga	stir, stir up, mix ingredients ( <b>Ukiukoroga mchele</b> , If you stir the rice, <b>Usipoukoroga mchele</b> , If you don't stir the rice. <i>See Language structure below for further explanation of the situational tense</i> )
-chemka	boil
-gandana	be stuck together, hardened fast (frozen)
mchanga	sand ( <i>pl. michanga</i> )
sivyo!	that's not so! not that way!
-acha	leave, leave behind (stop, quit, give up)
polepole	slowly, carefully
-toweke	disappear, vanish
kipofu	blind person ( <i>pl. vipofu</i> )
wakati	time ( <b>wakati + po</b> <i>in the verb</i> = when, while)
mbona	why, how come





<b>-bishana</b>	argue ( <i>lit.</i> disagree with each other, <i>cf.</i> <b>-bisha</b> , disagree)
<b>kelele</b>	noise, shouting ( <b>-piga kelele</b> , shout, make noise) ( <i>pl.</i> <b>makelele</b> )
<b>sivyo hivyo</b>	that's not right, not that way
<b>jinsi</b>	way, manner (kind, sort, species)
<b>ukweli</b>	truth, fact
<b>-onekana</b>	seem, appear (be seen/visible, <b>inaonekana</b> , it seems)
<b>mabishano</b>	dispute
<b>kazi bure</b>	wasted effort
<b>kadha</b>	( <i>adj.</i> ) certain, various ( <i>also</i> <b>kadha wa kadha</b> )
<b>-fundisha</b>	teach ( <b>tufundishe</b> , teach us)

## Language structure

### *The situational tense -ki-*

The situational or **-ki-** tense which is used in the dialogue describes an event which is seen as the background situation to a main event. This can either be a hypothetical, possible situation, in which case the **-ki-** tense can often be translated as an English if-clause, or a situation holding at the same time as the main event, in which case an English translation as a participial clause ('while doing X') is often appropriate. In general, hypothetical situations are introduced before the main predicate, while simultaneous situations are introduced after the main predicate:

**Ukimwona mama anapika wali utaona kwamba . . .**

If you see mother cooking rice you will see that . . .

**Ukiingia kwenye gari utaona mizigo yako imo ndani.**

If you get in the car you will see your luggage inside.

**Nilimwona akiingia kwenye gari.**

I saw him while he was getting in a car.

The hypothetical character of the situation can be reinforced by using the conjunctions **kama** or **ikiwa**, meaning 'if':

**Kama tukifanya haraka tutamaliza kazi yetu kabla ya saa kumi.**

If we hurry (make haste) we will finish our work before  
4 p.m.

Monosyllabic verbs do not take the stem marker with the **-ki-** tense:

**ukija** ... if/when you come ...  
**tukila** ... if/when we eat ...

There is no real negative counterpart to the **-ki-** tense. Often a negative relative of place is used to express negative hypothetical situations:

**Asipofika asubuhi tutaondoka.**

If she doesn't arrive in the morning, we will leave.

Sometimes a negative optative can be used:

**ukitaka usitake** ...  
 if you want or not ...

There are some commonly used phrases which are expressed in the **-ki-** tense, for example:

**Tukijaliwa.**  
*(lit. if we are granted)*

**Tutaonana tena tukijaliwa.**  
 If all goes well, we will meet again.

**Mungu akipenda.**  
*(lit. if God likes)*

**Mwaka huu nitakwenda Ulaya, Mungu akipenda.**  
 This year I will go to Europe, God willing.

## Exercise 1

Complete the sentences in the left-hand column with the appropriate ending in the right-hand column:

Kama ukienda shuleni	hawatakata vitabu hivi.
Mkija hapa kesho	wakila chakula.
Tuliwaona	Mungu akipenda.
Wasipofika shuleni kesho	mtapata pesa.
Mwaka ujao nitakwenda Afrika	utapata elimu.

## Exercise 2

Translate the short passage below into English:

Kama ukiingia jikoni utaona jinsi wapishi wanavyopika vyakula vya aina mbalimbali. Afadhali baadhi ya vyakula hivyo vichemshwe, vingine vichomwe, vibanikwe (*be grilled*) au vikaangwe (*be fried*). Jana niliwaona wapishi wakipika chakula cha wageni wa arusi. Ukifanya haraka utawaona kabla hawajamaliza kazi yao.

## Dialogue 2

*At present Ibrahim is working as an electrician at the broadcasting station in Dar es Salaam. There are some problems at work, and Ibrahim tries to explain this to his wife, Amani*

- 1 What is Ibrahim going to do on Sunday?
- 2 What has his wife, Amani, arranged to do on the day in question?
- 3 What does Amani tell him to do?

AMANI: Mbona inabidi ufanye kazi Jumapili. Si siku ya kupumzika?

IBRAHIM: Kuna kazi nyingi. Mwishoni mwa wiki iliyopita kulikuwa na shida nyingi kutokana na umeme uliokatwa mara kwa mara. Kwa sababu hiyo kuna shida na mkondo wa umeme kufika kompyuta na vyombo vingine vya umeme. Mimi ndiye mhandisi umeme, lazima niende kazini ili kufanya matengenezo.

AMANI: Ungaliniambia utakwenda kazini ningaliwaambia wazazi wangu kuwa tutawatembelea siku nyingine.

IBRAHIM: Na wewe ungaliniambia tutakwenda kuwatembelea wazazi wako nisingalikubali kwenda kazini Jumapili.

AMANI: Mpigie simu mkubwa wako ukamwambie wewe huwezi kufika kazini.

IBRAHIM: Haiwezekani bibi.

AMANI: Kwa nini?

IBRAHIM: Kwa ajili ya pesa. Ningekuwa na pesa za kutosha nisingekwenda kazini Jumapili. Tena, nataka kuwaonyesha wakubwa kuwa mimi ni mtu hodari wa kazi. Wakiniona kuwa mtu hodari nitapandishwa cheo na mshahara wangu utazidishwa vilevile. *Mtaka cha mvunguni sharti ainame.*

## Vocabulary

<b>-pumzika</b>	rest, take a break
<b>shida</b>	problem(s), difficulty(-ies)
<b>umeme</b>	electricity
<b>-katwa</b>	be cut
<b>mara kwa mara</b>	from time to time
<b>mkondo</b>	current
<b>vyombo</b>	equipment, vessels, tools
<b>mhandisi umeme</b>	electrician, electrical engineer
<b>matengenezo</b>	repairs, maintenance
<b>Ungali ... ningali ...</b>	If you had ... I would have ... ( <i>See Language structure below for explanations on the use of the conditional tense -ngali-</i> )
<b>nisingali ...</b>	I wouldn't have ... ( <i>see Language structure</i> )
<b>haiwezekani</b>	it is impossible
<b>Ningekuwa na ...</b>	If I had ... ( <i>see Language structure</i> )
<b>-a kutosha</b>	( <i>adj.</i> ) enough
<b>-onyesha</b>	show, demonstrate
<b>hodari</b>	( <i>adj.</i> ) hardworking, serious (brave, courageous)
<b>-pandishwa</b>	be raised, hoisted, uplifted
<b>cheo</b>	rank, position, status ( <i>pl.</i> <b>vyeo</b> )
<b>mshahara</b>	salary, pay, wage ( <i>pl.</i> <b>mishahara</b> )
<b>-zidishwa</b>	be increased (be multiplied, augmented, magnified, enlarged)
<b>mvunguni</b>	under the bed, in the space beneath ( <i>cf.</i> <b>mvungu</b> , the space beneath)
<b>-inama</b>	bend (stoop/lean/bow)



## Language point

### *Proverb*

**Mtaka cha mvunguni sharti ainame** (*lit.* ‘The one wanting what’s under the bed has to stoop’) ‘Good things are not easily obtained, one must strive to get them.’ **Mtaka** combines the **m-**prefix of the M-WA class with the verb **-taka**, a ‘wanter’ if we could say this in English. The **cha** with no noun of reference refers to **kitu**, ‘thing’. **Mvungu** is the space beneath a bed. The people of Zanzibar often use this space as a storage area for small items such as, cooking utensils, provisions, or valuables.

## Language structure

### *The conditional tenses -nge- and -ngali-*

We have already seen that hypothetical situations can be expressed by using the **-ki-** tense. However, the **-ki-** tense cannot be used for those hypothetical situations which are highly unlikely to, or in fact cannot, become reality – such as counter-factual situations. For these situations, the **-nge-** and **-ngali-** tenses are used. The **-nge-** tense expresses highly unlikely or improbable, but nevertheless possible situations:

**Ningekuwa na pesa nyingi ningekuoa.**

If I had a lot of money, I would marry you.

**Angefika mapema, tungeondoka pamoja.**

If she arrives early, we would leave together.

Note that in Swahili both clauses, the ‘condition’ and the ‘consequence’, are marked with the conditional tense **-nge-**.

Monosyllabic verbs (such as **kuwa** in the example above) take the stem marker:

**Angekunywa dawa angeona nafuu.**

If he drank medicine, he would feel better.

The negative of the **-nge-** tense is formed by placing the negative marker **-si-** before it:

**Nisingejua nisingekuja.**

If I didn’t know, I would not come.

In contrast to **-nge-**, **-ngali-** expresses counter-factual situations, those which can under no circumstances be true. This distinction is similar to the one expressed in the English distinction between the two conditional forms ‘would marry’ and ‘would have married’, although the Swahili distinction is less strict than the English:

**Angalifika mapema, tungaliondoka pamoja.**

If she had arrived early, we would have left together.

**Tusingalikula chakula chote, angalitupikia.**

If we hadn’t eaten all the food, he would have cooked for us.

### Exercise 3

Complete the sentences in the left-hand column with the appropriate ending in the right-hand column:

Tungalikata tiketi jana	ningemwona daktari.
Ningekuwa mgonjwa	asingalikuwa mgonjwa.
Asingalitumia sabuni mpya	tungefika pamoja.
Wasingeondoka mapema	tungalikwenda Tanga leo.

### Exercise 4

Translate sentences 1–6 into Swahili:

- 1 If I had money, I would go to Tanzania.
- 2 If you were to buy the tickets, we would leave today.
- 3 If she ate the food, she would feel better.
- 4 If I didn’t eat the food, I wouldn’t feel better.
- 5 If they had arrived yesterday, we would have stayed together.
- 6 If you hadn’t cooked the food, our guests wouldn’t have come here.

### Dialogue 3

*Amos and his brother, Mwesi, are arguing over the use of their father’s car*

MWESI: Huwezi kulitumia gari leo.

AMOS: Kwa nini?

MWESI: Nina shughuli nyingi leo.

- AMOS: Je, una shughuli gani?  
 MWESI: Kwanza, nitamsindikiza rafiki anayekwenda uwanja wa ndege. Halafu nitakwenda dukani kununua nguo. Baada ya kufanya mambo hayo nitampitia mchumba wangu.  
 AMOS: Ungaliniambia utalitumia gari lake baba kwa siku nzima ningalimwomba mjomba gari lake.  
 MWESI: Ungaliniambia unataka kulitumia gari ningalifanya mipango mingine.  
 AMOS: Badala ya kugombana sisi tusaidiane. Hebu, nahitaji msaada wako.  
 MWESI: Haya basi! Afadhali tupatane. Leo nitamsindikiza rafiki yangu na kesho nitafanya mambo hayo mengine. Utaweza kulitumia gari leo, sawa?  
 AMOS: Sawasawa. Heri tukubaliane kuliko kubishana.

## Vocabulary

- shughuli** business, pursuits, preoccupations, activity  
**-sindikiza** see someone off, accompany a visitor part way, escort someone  
**-pitia** pass by, pay a passing visit (pass out of mind/ be overlooked)  
**badala ya** instead of  
**-gombana** quarrel, argue (*lit.* quarrel/argue with each other. *See Language structure below for further explanation of this verb*)  
**-saidiana** help each other (**tusaidiane**, let's help each other. *See Language structure*)  
**-patana** get along well, be compatible (agree on something, **tupatane**, let's get along. *See Language structure*)  
**-kubaliana** be in agreement, agree with each other (**Heri tukubaliane**, It's better to agree. *See Language structure*)

## Language structure

### *The reciprocal extension*

The reciprocal extension is comparatively easy to handle, both in terms of shape and in terms of meaning. The form of the reciprocal extension is **-an-** and it never varies. The meaning of the

extension can be roughly translated as ‘each other’, as for example in **kuta** ‘meet’ and **kutana** ‘meet each other’:

**Asha alimkuta Rashid.**

Asha met Rashid.

**Asha na Rashid walikutana.**

Asha and Rashid met each other.

**Amos anakubali.**

Amos agrees.

**Amos anamkubalia Mwesi.**

Amos agrees with Mwesi. (*with applicative extension*)

**Amos na Mwesi wanakubaliana.**

Amos and Mwesi agree with each other.

Since the meaning of the extension implies that the action of the verb is carried out by two or more people (doing something with, or to, each other), it is often used with a plural subject:

**Tutaonana.**

We will see each other/meet.

**Watu hawa wanagombana.**

These people are quarrelling.

Sometimes a singular subject can be used when a second noun with the preposition **na** follows the verb:

**Nitakutana naye.**

I will meet with him/her.

**Anasaidiana nami.**

She is helping me.

Be careful to use the applicative extension if you want to say that two people are doing things for or with each other:

**Wanapikiana.**

They are cooking for each other.

## Exercise 5

By using the reciprocal extension, make sentences which say that the people to the left do the action to the right for, with, etc., each other:



E.g. Q. **Amos, Kathy** kuta  
 A. **Amos na Kathy** wanakutana

- |                                 |                      |
|---------------------------------|----------------------|
| 1 <b>Amos, Kathy</b>            | <b>penda</b>         |
| 2 <b>Sandra, Leila</b>          | <b>ona</b>           |
| 3 <b>Mamantilie, binti yake</b> | <b>saidia</b>        |
| 4 <b>Subira, Amos</b>           | <b>uliza maswali</b> |
| 5 <b>Wasichana, wavulana</b>    | <b>leta zawadi</b>   |

## Language use

### *Expressing your point of view*

Some useful verbs:

**-kubali**  
agree

**-pinga**  
disagree, oppose

**-kubaliana na**  
agree with

**-gomba**  
scold, argue, disagree

**-bisha**  
disagree

**Sikubali.**  
**Nakubaliana naye.**  
**Nabisha!**

I don't agree.  
I agree with him/her.  
I disagree!

**Kwa nini tunagombana?**

Why are we arguing?

Useful phrases and structures:

**kwanza**  
first, firstly

**halafu**  
then, later on

**tena**  
again, still, besides

**pia/vilevile**  
also

**mbali na**  
apart/aside from

**mwishowe**  
finally, in the end

**licha ya**  
aside from, besides,  
let alone, despite

**badala ya**  
instead of

**Kwanza, tunabishana.**

Firstly, we disagree.

**Halafu, wanagombana.**

Then, they quarrel.

**Nabisha pia.**

I also disagree.

**Badala ya kugombana, tujaribu kupatana.**

Instead of quarrelling, let's try to get along.

**Verbs expressing your thoughts:****-dhani/-fikiri**

think

**-waza**

think, imagine, conceive  
(meditate)

**Nimewaza juu ya ugomvi wetu.**

I have pondered over our argument.

**Other useful words:****maoni**

views, opinion

**mawazo**

thoughts, ideas

**hisia**

feelings

**hakika**

fact, certainty

**shaka**

doubt

**wazi**

(*adj.*) clear, evident, open, overt  
(empty, vacant)

**Maoni yangu ni wazi.**

My feelings are clear.

**Sipendi mawazo hayo.**

I don't like those ideas.

**Una hakika?**

Are you sure?

**Ni hakika.**

It is a fact.

**Hapana shaka.**

There's no doubt.

**Bila shaka.**

Without doubt.

***Expressing more complex arguments*****lakini/walakini**

but, however

**bali**

on the contrary, rather, but,  
however

**upande**

side (sector, direction)

**hivyo**

thus, in that way

**hali**

while, seeing that, when

**Una mawazo mazuri lakini sikubaliani nayo.**

You have some good ideas but I don't agree with them.

**Bali, nakubaliana na mawazo yao.**

However, I agree with their ideas.

**Kwa upande wangu, nafikiri yote ni sawa.**

As for myself, I think all are right.

**Hata hivyo, maoni yetu yanatofautiana.**

Even so, our views are different.

**Exercise 6**

Say in Swahili:

- 1 I don't agree. I agree with her.
- 2 Let's agree with each other.
- 3 Why are we arguing? Let's not argue.
- 4 Firstly, I disagree. Then we quarrel.
- 5 Instead of quarrelling, you (*pl.*) should try to get along.
- 6 I have pondered over our argument, I don't like your ideas.
- 7 My views are clear but you don't like my ideas.
- 8 Are you sure? Is it a fact?
- 9 I'm not sure. It isn't a fact.
- 10 Without doubt you have some good ideas. Now we agree.

**Reading****Urithi**

Ikiwa marehemu hakufanya wasia kabla ya kufariki dunia ndugu zake hawatajua vipi wataweza kujigawia mali yake. Jambo kama hilo huleta 'taabu za nyumbani', yaani ndugu hao watabishana na kugombana.

Katika hali kama hiyo, baada ya mali yake marehemu katwanyika, baadhi ya ndugu wataridhika na wengine watajiona

wamedanganywa. Hisia kama hizo zinaweza kuwafanya ndugu kutozungumzana kwa muda mrefu au hata milele.

Bali, kama mtu akifanya wasia yake kabla hajafa, ndugu zake watajua barabara warithi wake ni nani.

## Vocabulary

<b>urithi</b>	inheritance/heritage
<b>marehemu</b>	deceased person
<b>wasia</b>	solemn wish, parting advice, last will and testament
<b>-fariki</b>	die, leave for good ( <b>-fariki dunia</b> , <i>lit.</i> leave the earth)
<b>-gawia</b>	divide among, distribute to ( <b>jigawia</b> , divide among one's selves, share)
<b>mali</b>	wealth, property, goods
<b>-gawanyika</b>	be divided
<b>-ridhika</b>	be satisfied
<b>-danganywa</b>	be deceived/cheated
<b>hisia</b>	( <i>also hisi</i> ) feeling(s), sentiment(s), sensation(s)
<b>milele</b>	forever, eternally
<b>barabara</b>	perfectly, flawlessly, precisely, exactly
<b>warithi</b>	inheritors ( <i>sing.</i> <b>mrithi</b> )

# 12 Hadithi na magazeti

## Stories and newspapers

**In this unit you will learn:**

- how to tell a story using the narrative tense **-ka-**
- how to read newspaper headlines using the **-a-** tense
- how to refer to manner and time

### Dialogue 1

*Kathy tells Ibrahim a story*

- 1 When Kathy was a young child what did her father do?
- 2 What happened to Kathy after hearing the stories?
- 3 Kathy liked a particular story, what was this story about?

KATHY: Nilipokuwa mtoto mdogo kila jioni, kabla sijalala, babangu hunisimulia hadithi za watoto. Baada ya kusikia hadithi hizo, mara nyingi niliota ndoto. Hadithi mojawapo niliyoienda sana ilikuwa ndiyo hadithi ya *Sungura na Kobe*.

IBRAHIM: Vilevile nilipokuwa mtoto mdogo nilisimuliwa na wazee wangu hadithi hiyohiyo, lakini nimesahau mambo yali-yotokea.

KATHY: Nakumbuka hadithi hiyo. Unataka nikusimulie hadithi ya *Sungura na Kobe*?

IBRAHIM: Ndiyo.

KATHY: *Sungura na Kobe* ndiyo hadithi inayohusu shindano la mbio baina ya sungura anayejisifu na kobe mwerevu:

*Hapo zamani Sungura alipokuwa akitembeatembea kujisifu, akamkuta Kobe ambaye alikuwa akila majani. Baada ya ku-amkiana, Sungura akatoa changamoto washindane kwenye shindano la mbio.*

'Sawa!' akakubali Kobe. 'Wewe ni mwerevu, lakini mimi ni mwerevu zaidi kuliko wewe,' akajisemea. Kisha Kobe akamwongoza Sungura kilimani. Kobe alipochukua muda mrefu kufika kwenye kilele cha kilima Sungura akajisemea, 'Bila shaka Kobe atashindwa. Kobe huyu hawezi kutembea vizuri.'

Kobe alipomfikia Sungura akamwuliza, 'Je, uko tayari?'

'Ndiyo, niko tayari! Ndiye mimi anayekungojea!' akasema Sungura bila uvumulivu wowote.

'Twende!' alisema Kobe. Papo hapo aliingia ndani ya gomba lake akashuka kilimani kama jiwe. Sungura alikuwa akikimbia mbio awazavyo lakini hakuweza kumfikia Kobe.

Sungura, alipofika katikati ya kilima alisimama kumtazama Kobe ambaye alikuwa ameshafika chini. Sungura alishindwa.

**IBRAHIM:** Sikumbuki matokeo kama hayo. Hadithi ya Sungura na Kobe nilivyokumbuka inatofautiana na ile uliyonisimulia leo.

**KATHY:** Ndiyo. Kuna masimulizi mbalimbali ya hadithi hiyo, lakini maadili ya hadithi ni sawa. Kama methali inavyosema: 'Aliyeko juu mngojee chini.'

## Vocabulary

<b>nilipokuwa</b>	when I was ( <b>ni + li + po + kuwa</b> )
<b>-lala</b>	sleep/lie down
<b>-simulia</b>	tell a story, narrate
<b>-ota</b>	dream (grow)
<b>ndoto</b>	dream(s) ( <b>-ota ndoto</b> , dream a dream)
<b>-mojawapo</b>	( <i>adj.</i> ) one of ( <b>hadithi mojawapo</b> , one of the stories, <b>kitabu kimojawapo</b> , one of the books)
<b>sungura</b>	hare(s), rabbit(s)
<b>kobe</b>	tortoise ( <i>pl.</i> <b>makobe</b> )
<b>-tokea</b>	happen, occur, appear
<b>-husu</b>	concern, relate to, about
<b>mbio</b>	speed, rate of speed, sprint
<b>-jisifu</b>	boast, praise oneself
<b>mwerevu</b>	someone who is sharp, clever, cunning
<b>hapo zamani</b>	once upon a time
<b>-tembea</b>	walk, walk around ( <b>-tembeatembea</b> , walk here and there, wander)

<b>akamkuta Kobe</b>	and then he came across the Tortoise, ( <b>a + ka + m + kuta</b> , see <i>Language structure for explanation of the -ka-</i> tense used here)
<b>majani</b>	leaves/grass ( <i>sing. jani</i> )
<b>baada ya</b>	after
<b>-amkiana</b>	greet each other ( <i>cf. -amkia</i> , greet someone)
<b>changamoto</b>	challenge
<b>woga</b>	fear, cowardice
<b>juu ya</b>	concerning, about (on, on top of, above: <b>juu yako</b> , concerning you)
<b>-ogopesha</b>	frighten, scare
<b>kisha</b>	then/finally/afterwards
<b>-semea</b>	speak to/for ( <b>-jisemea</b> , say to oneself)
<b>-ongoza</b>	lead, guide, show the way
<b>alipochukua</b>	when he took ( <b>a + li + po + chukua</b> , see <i>Language structure for explanation</i> )
<b>kilele</b>	summit, peak
<b>-fikia</b>	arrive at, catch up with
<b>uko tayari?</b>	are you ready?
<b>niko tayari</b>	I am ready
<b>-ngojea</b>	wait for
<b>uvumulivu</b>	patience, tolerance
<b>papo hapo</b>	there and then
<b>ndani</b>	inside
<b>gamba</b>	shell ( <i>pl. magamba</i> )
<b>-shuka</b>	descend, go down (get off, disembark)
<b>jiwe</b>	stone ( <i>pl. mawe</i> )
<b>-kimbia</b>	run (run away, flee, escape, <b>-kimbia mbio</b> , sprint)
<b>-wezavyo</b>	as possible ( <b>alikuwa akikimbia mbio awezavyo</b> , he was running as fast as he could)
<b>-simama</b>	stop (stand, rise up)
<b>-tazama</b>	look at, watch, gaze at
<b>chini</b>	on the ground, at the bottom, down, under, below
<b>matokeo</b>	outcome, result
<b>nilivyokumbuka</b>	the way/how/as I remembered ( <b>ni + li + vyo + kumbuka</b> , see <i>Language structure</i> )
<b>-tofautiana</b>	be different
<b>masimulizi</b>	narrations, tale (accounts, versions)
<b>maadili</b>	ideals, ethics (morals)

## Language point

### *Proverb*

**Aliyeko juu mngojee chini** ‘He who thinks that he is standing should be careful not to fall down’ (*lit.* ‘He who is on top wait for him below’). This proverb is sometimes said of somebody who is very sure of his success. Being a fast-footed animal, the Hare was sure of his success over the slow-moving Tortoise; however, he didn’t bargain on being outwitted by the clever Tortoise.

## Language structure

### *The -ka- tense*

The **-ka-** tense which is used in the story in forms such as **akamwambia** and **akakubali** is often found in stories and other narrative texts. It is sometimes called ‘subsecutive’ tense, as it expresses the fact that an action follows another (is subsequent to it). As in the text about the Hare, the **-ka-** tense most frequently occurs following a verb in the **-li-** tense, and can then be translated as ‘... and then ...’:

**Sungura aliamka, akatembea, akala.**

The hare got up, and (then) took a walk, and (then) ate.

As you can see from **akala**, monosyllabic verbs do not take the stem marker in this tense.

Another frequent use of the **-ka-** tense is after imperatives or optatives (see Unit 5, Dialogue 1), when you are asked to do two actions, one after the other:

**Nenda kalale.**

Go and sleep!

**Njoo ukapimwe.**

Come and get tested!

Here the verb takes the **-e** ending as in the optative.



## Exercise 1

Use the fragments given below and construct a story using the **-ka-** tense where appropriate. Be careful not to use the stem marker.

E.g.

**Jana**  
**Kuku**  
**kwenda sokoni**  
**kununua chakula**  
**kurudi nyumbani**  
**kula chakula.**

Using the **-ka-** tense, the above would narrate as:

**Jana Kuku alikwenda sokoni akanunua chakula, akarudi nyumbani akala chakula.**

Yesterday the Chicken went to the market and bought some food, and then he returned home and ate the food.

Now your turn . . .

**-ibia** = steal from, rob (*cf.* **-iba**, steal)

Siku moja  
Paka  
kuamka mapema  
kunywa chai  
kwenda sokoni  
kununua samaki.  
Kabla ya kula samaki  
kumkuta Sungura  
kumwamkia  
kusema 'Kwa Heri'.  
Baada ya Sungura kuondoka,  
Paka kuona kwamba Sungura yule alimwibia samaki.

## Exercise 2

Now translate the narrative from Exercise 1 into English.

## Dialogue 2

*Amos and Leo are talking about a newspaper article*

- 1 Where did the accident happen?
- 2 How did the accident happen?
- 3 How many wedding guests were travelling in the bus?

AMOS: Je, umeisoma makala katika gazeti kuhusu ajali baina ya basi na treni huko Bara Hindi?

LEO: Bado sijaisoma. Makala hiyo inasema nini?

AMOS: Ngoja, nitakusomea jinsi makala ilivyoandikwa katika gazeti. Kichwa cha habari kinasema: *WATU THELATHINI NA MMOJA WAFWA AMBAPO BASI LAGONGANA NA TRENI:*

*Watu wasiopungua thelathini na mmoja wamekufa ambapo basi lililojaa wageni wa arusi likagongana na treni kwenye tambuka reli (yaani makutano ya barabara na reli) isiyo na mlinzi kaskazini mwa Bara Hindi. Watu arobaini na tisa wengine walipata majeraha na wanatibiwa katika hospitali mjini Kheri. Polisi mmoja asema, wengi wao waliojeruhiwa walikuwa Waislamu maskini waliofanya kazi mashambani au kufanya kazi ndogondogo. Hilo basi lilikuwa na idadi ya viti sitini, lakini likawa limejaa wageni wa arusi themanini.*

LEO: Jamani! Ni msiba mkubwa.

AMOS: Ndiyo. Bwana arusi na biarusi siku zote watakumbuka msiba huo. Wataikumbuka siku yao ya arusi kwa huzuni kubwa sana.

## Vocabulary

<b>makala</b>	article, written paper for presentation
<b>ajali</b>	accident
<b>jinsi + vyo</b> ( <i>in verb</i> )	as, how, the way
<b>kichwa cha habari</b>	headline, heading ( <i>lit. head of news, pl. vichwa vya habari</i> )
<b>-fa</b>	die ( <b>wafa</b> , they die. <i>Monosyllabic verb, doesn't take a stem marker with the a- tense; see Language structure</i> )
<b>-gongana</b>	collide with, bump into one another ( <i>from gonga, collide</i> )

<b>-pungua</b>	decrease, diminish ( <b>-siopungua</b> , not less than, at least)
<b>-jaa</b>	be full
<b>tambuka reli</b>	level crossing
<b>isiyo na</b>	that (level crossing) does not have, is without
<b>mlinzi</b>	guard, watchman, bodyguard, defender ( <i>pl. walinzi</i> )
<b>kaskazini</b>	the north
<b>majeraha</b>	injuries, wounds ( <i>sing. jeraha</i> )
<b>-tibiwa</b>	be medically treated
<b>-jeruhiwa</b>	be injured, wounded
<b>maskini</b>	poor person, unfortunate person, object of pity
<b>kazi ndogondogo</b>	odd jobs, small chores ( <i>lit. work smallsmall</i> )
<b>idadi</b>	total, number
<b>msiba</b>	bereavement, sorrow, misfortune/heartbreak
<b>siku zote</b>	always, all days
<b>huzuni</b>	sadness

## Language structure

### *The -a- tense*

There are three verbs in the dialogue which are used in the **-a-** tense:

<b>wafa</b>	they die
<b>lagongana</b>	it ( <b>basi</b> ) hit
<b>asema</b>	s/he says

The **-a-** tense is the last tense encountered in this course. Like the **-na-** tense, it refers to the present, but it is less frequent than the **-na-** tense. As can be seen in the dialogue, it is often found in newspaper articles and headlines. The **-a-** tense is formed by combining the subject concord with the **-a-** tense marker. For some subject concords, this leads to changes into the following forms:

Participants:

<b>ni + a = na</b>	<b>nasema</b>	<b>u + a = wa</b>	<b>wasema</b>
	I say		you say

<b>tu + a = twa</b>	<b>twasema</b> we say	<b>m + a = mwa</b>	<b>mwasema</b> you ( <i>pl.</i> ) say
M-WA Class <b>a + a = a</b>	<b>asema</b> s/he says	<b>wa + a = wa</b>	<b>wasema</b> they say
JI-MA Class <b>li + a = la</b>		<b>ya + a = ya</b>	
N Class <b>i + a = ya</b>		<b>zi + a = za</b>	
M-MI Class <b>u + a = wa</b>		<b>i + a = ya</b>	
KI-VI <b>ki + a = cha</b>		<b>vi + a = vya</b>	
U <b>w + a = wa</b>			
PA-KU-MU <b>pa + a = pa</b> <b>ku + a = kwa</b> <b>mu + a = mwa</b>			
KU <b>ku + a = kwa</b>			

As can be seen from **wafa**, above, monosyllabic verbs do not take the stem marker in the **-a-** tense.

The 1st person singular form is identical to the contracted form of the **-na-** present: **ni + na = na**, in, for example, **nasoma** (see Unit 1, Dialogue 2). However, because monosyllabic verbs do take the stem marker **-ku-** in the **-na-** tense, but not in the **-a-** tense, these verbs can be distinguished: **nakuja** is the contracted form of the **-na-** tense, **naja** has the **-a-** tense.

### Exercise 3

Join the noun on the left with the appropriate verb in the **-a-** tense on the right:

- |                    |                           |
|--------------------|---------------------------|
| 1 michungwa mitano | asema.                    |
| 2 hadithi          | waja kutembelea Tanzania. |
| 3 treni nyingi     | yaharibiwa na moto.       |
| 4 mlinzi           | yasimuliwa na mamake.     |
| 5 wageni wengi     | zachelewa.                |

### Exercise 4

Change the **a-** tense of the verbs in the following newspaper headlines to the **-na-** tense:

- 1 Bei ya pombe, soda, sigara yapanda.
- 2 Serikali yakubali mpango wa chuo kikuu.
- 3 Jambiani yashindwa na Makunduchi.
- 4 Watu wa Mwanza wafurahia hospitali mpya.
- 5 Vitabu vya zamani vyauzwa na chuo kikuu.

### Dialogue 3

*Subira and Victoria are in their room. While Victoria is doing the washing up, her room-mate is reading her the newspaper*

- 1 Has Victoria read the newspaper?
- 2 According to the newspaper, what did the Kenyan runners achieve at the Olympics?
- 3 Apart from the usual articles, what else does Victoria ask her roommate to read to her?

SUBIRA: Gazeti hili lina makala nyingi za kuvutia.

VICTORIA: Sijalisoma bado. Tafadhali nismee.

SUBIRA: Vichwa vya habari katika ukurasa wa kwanza vinasema:  
*MEYA AFURAHIA 'MTOTO MPYA'/SHULE  
NYINGINE YACHOMWA MOTO/HALI YA HEWA  
YAATHIRI KILIMO/MWANAMKE ATUHUMIWA  
KUMNYONGA MTOTO WAKE.*

VICTORIA: Haki ya Mungu! Siku hizi kuna habari mbaya zaidi katika magazeti kuliko habari nzuri. Pengine ninaposoma gazeti ninakuwa nimejaa huzuni. Ukurasa wa nyuma unasema nini?

SUBIRA: Vichwa vya habari katika ukurasa wa nyuma vinasema:  
*MABONDIA WATAMBIANA, WAKENYA  
 WAVUMA, BENDI ZACHANGIA TIMU YA  
 MPIRA WA KIKAPU IENDE NAIROBI*

VICTORIA: ‘Wakenya wavuma’, ilitokea nini?

SUBIRA: Katika michezo ya Olimpiki wakimbiaji wa Kenya walionyesha ubingwa wao na kutwaa nafasi nne za kwanza katika mbio za masafa marefu. Kwa hakika watakaporudi nyumbani wakimbiaji Wakenya hao watalakiwa vizuri na raia wenzao.

VICTORIA: Nyota zinasema nini?

SUBIRA: Kila ninaposoma nyota zinatoa habari mbaya.


VICTORIA: Inategemea jinsi unavyozifahamu.

SUBIRA: Una alama ya nyota gani?

VICTORIA: Alama yangu ya nyota ni Mapacha.

SUBIRA: Katika gazeti hili shauri linasema: ‘Tegemea kupata upinzani katika kazi na shughuli zako. Upo mpango ambao unafanywa ili kuharibu maendeleo yako ...’

VICTORIA: Basi! Wiki hii nitakuwa mwangalifu!



## Vocabulary

<b>huku</b>	while (here, hereabouts)
<b>vyombo vya jikoni</b>	kitchenware
<b>-a kuvutia</b>	( <i>adj.</i> ) attractive, impressive, fascinating
<b>ukurasa</b>	page ( <i>pl.</i> <b>kurasa</b> )
<b>meya</b>	mayor of a city

<b>-furahia</b>	be happy about
<b>-chomwa</b>	be roasted/burnt (be pierced/stabbed)
<b>hali ya hewa</b>	the weather
<b>-athiri</b>	affect, influence (infect, harm, spoil, damage)
<b>kilimo</b>	agriculture
<b>-tuhumiwa</b>	be suspected (of)
<b>-nyonga</b>	strangle, hang someone
<b>haki</b>	justice/right(s) ( <b>Haki ya Mungu</b> , Honest to God, <i>lit.</i> the rights of God/God's justice)
<b>pengine</b>	sometimes (perhaps, otherwise)
<b>ninaposoma</b>	when I am reading ( <b>ni + na + po + soma</b> , <i>see following Language structure</i> )
<b>nyuma</b>	back, rear
<b>mabondia</b>	boxers ( <i>sing.</i> <b>bondia</b> )
<b>-tambiana</b>	brag/boast to one another
<b>-vuma</b>	be the talk of the town, cause a stir (roar, bellow, buzz)
<b>bendi</b>	musical band
<b>-changia</b>	contribute to (collect, solicit for, kiss)
<b>timu ya mpira</b>	basketball team
<b>wa kikapu</b>	
<b>wakimbiaji</b>	runners ( <i>sing.</i> <b>mkimbiaji</b> )
<b>ubingwa</b>	championship, expertise
<b>-twaa</b>	take, pick up, take over (capture, occupy)
<b>masafa</b>	range, distance
<b>watakaporudi</b>	when they will return ( <i>see Language structure</i> )
<b>-lakiwa</b>	be welcomed, received (passive of <b>-laki</b> )
<b>raia</b>	citizen(s)
<b>nyota</b>	star(s)
<b>alama</b>	sign, symbol, mark, pockmark, scar
<b>mapacha</b>	twins, Gemini star sign
<b>shauri</b>	advice
<b>upinzani</b>	opposition
<b>mwangalifu</b>	a careful/attentive person ( <i>pl.</i> <b>waangalifu</b> )

## Language structure

### *Relatives of manner and time*

Relatives of manner and time are formed like normal relatives, usually tensed relatives (cf. Unit 10, Dialogue 1), but they have a special usage since they can be used to elaborate on when and how an action is taking place. The relative of time is formed like a locative relative with the referential concord of the PA class. Relatives of manner are formed with the referential concord of the plural of the KI-VI class:

**Alipoamka ...**                      When he got up ...  
**Nilivyosema ...**                    As I have said ...

In dialogue 1 of this unit, Kathy uses a temporal relative when saying

**Nilipokuwa mtoto mdogo ...**  
 When I was a little child ...

In these relatives, the referential concord does not have an overt head-noun that it refers to. The relative of time exploits a metaphorical extension of the concept of place to the concept of time and can be used with a head-noun such as (the U-class noun) **wakati**, 'time'. With an overt head-noun such as **mahali**, 'place', the referential concord refers to place, and the relative becomes locative:

**Wakati nilipoamka ...**      At the time when I got up ...  
**Mahali nilipoamka ...**      At the place where I got up ...

In the relative of manner, the plural KI-VI class referential concord can be used because the plural KI-VI class can be used to form manner adverbs (for example **niliamka vizuri** 'I got up well' – we will not deal with this aspect of the KI-VI class in this course). It is sometimes used with the N-class head-noun **jinsi**, 'kind, way', or with the conjunction **kama**, 'as, how':

**Jinsi alivyoadika ...**      The way in which he wrote ...  
**Kama ulivyosema ...**      As you said ...

Relatives of manner and time are also formed with the **amba**-relative, and can be found with the general relative, as for example in the following proverb with the verbs **-lea**, 'bring up', and **-kua** 'grow up':



**Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.**

As you bring up a child, a child will grow up.

**Exercise 5**

Decide which of the following relatives are relatives of manner, relatives of time, or neither:

- 1 Vitabu *alivyonununa* ni vizuri.
- 2 Tulimkuta nyumbani *alipokaa*.
- 3 Kama *walivyosema* jana, watarudi kesho tu.
- 4 *Mtakapofika* Dar, mtaiona hoteli ya 'New Africa' upande wa kulia.
- 5 Alipika chakula wakati *nilipoamka*.
- 6 Maneno yale *uliyotumia* hayapendezi.

**Exercise 6**

Fill in the appropriate relative of manner, time, or other, which has been omitted in the passage below:

Leo asubuhi wakati nili\_\_\_\_amka nikasoma gazeti. Nilisoma habari za mchezo wa mpira lakini sikupenda jinsi habari hizo zili\_\_\_\_andikwa na mwandishi wa habari. Baadaye, nilikwenda dukani ana\_\_\_\_fanya kazi rafiki yangu. Baada ya kumtembelea rafiki yangu, nilikwenda mahali ali\_\_\_\_kaa mwalimu wangu lakini hakuwapo nyumbani. Wakati nili\_\_\_\_rudi nyumbani kwangu nikamwona mwalimu wangu amesimama mlangoni. Baada ya kuamkiana, mwalimu alinipa vitabu nili\_\_\_\_taka.

**Reading****Yaliyomo**

Yapo magazeti ya aina mbalimbali yanayouzwa Tanzania na Kenya. Baadhi ya magazeti hayo yanaandikwa kwa Kiswahili na mengine (kama vile *Daily Nation*) kwa Kiingereza. Baadhi ya hayo yanayojulikana sana ni: *Nipashe*, *Majira*, *Rai*, *Mfanyakazi* na *Uhuru*, (ambayo huchapishwa mjini Dar es Salaam, Tanzania) na *Taifa Leo* (ambalo huchapishwa mjini Nairobi, Kenya).

Magazeti hayo huwa na sehemu zifuatazo: habari za nyumbani (yaani habari kutoka mikoani), habari za kitaifa na za kimataifa, na habari za biashara (ambazo huhusikana na soko la hisa, bei za mazao, na viwango vya kubadilisha pesa). Pia kuna habari za matukio mahakamani (katika gazeti la *Taifa Leo* sehemu hii huitwa ‘Macho Yetu Mahakamani’, na katika gazeti la *Rai* huitwa ‘Sheria’), ‘Habari za Ulimwengu’, ‘Makala Maalumu’, na sehemu zinazohusikana na ‘Watu na Jamii’, Barua (yaani barua kwa Mhariri), na tanzia.

Licha ya matangazo ya kawaida, zipo sehemu zinazohusikana na burudani, kama vile: ‘Wasanii wa Tarab’ na wasanii wa muziki wa aina mbalimbali; hadithi na mashairi (katika gazeti la *Uhuru* huitwa ‘Maoni ya Washairi’); vipindi vya redio, vya televisheni na vya sinema; michezo (gazeti la *Uhuru* lina sehemu inayoitwa ‘Michezo Katika Picha’); na hatimaye katuni (yaani picha za kuchekecha) na chemshabongo/mafumbo ya maneno.

## Vocabulary

<b>yaliyomo</b>	table of contents
<b>mikoa</b>	regions, states, provinces ( <i>sing.</i> <b>mkoa</b> – <b>mikoani</b> , in the regions)
<b>-a kitaifa</b>	( <i>adj.</i> ) national
<b>-a kimataifa</b>	( <i>adj.</i> ) international
<b>biashara</b>	business, commerce, trade
<b>-husikana na</b>	be concerned with, be relevant to
<b>hisa</b>	stock(s), share(s)
<b>mahakama</b>	court of law ( <b>mahakamani</b> , in the court)
<b>sheria</b>	law(s); justice
<b>ulimwengu</b>	the world, the universe, creation
<b>maalum(u)</b>	( <i>adj.</i> ) special, famous
<b>jamii</b>	society, community
<b>mhariri</b>	editor
<b>tanzia</b>	obituary(-ies)
<b>matangazo</b>	announcements, advertisements ( <i>sing.</i> <b>tangazo</b> )
<b>burudani</b>	entertainment, recreation
<b>wasanii</b>	artists, painters, sculptors, authors, composers, technicians ( <i>sing.</i> <b>msanii</b> )
<b>mashairi</b>	poems ( <i>sing.</i> <b>shairi</b> )
<b>washairi</b>	poets ( <i>sing.</i> <b>mshairi</b> )
<b>vipindi</b>	period of time, programme on radio/tv (teaching period)

<b>katuni</b>	cartoon(s)
<b>-chekesha</b>	be funny/amusing (make someone laugh)
<b>chemshabongo</b>	crossword(s) ( <b>chemsha</b> , cause to boil; <b>bongo</b> , <i>colloquial for brains</i> )
<b>mafumbo ya maneno</b>	crosswords ( <i>sing.</i> <b>fumbo la maneno</b> )

## Exercise 7

Answer these questions about the Reading in Swahili:

- 1 Je, gazeti hilo la *Daily Nation* linachapishwa kwa Kiswahili?
- 2 Je, magazeti hayo ya *Majira* na *Mfanyakazi* yanachapishwa mjini Nairobi, Kenya?
- 3 Magazeti ya *Nipashe* na *Rai* huchapishwa wapi?
- 4 Gazeti la *Taifa Leo* huchapishwa wapi?
- 5 Habari za matukio mahakamani huitwa nini katika gazeti la *Taifa Leo*?
- 6 Habari za matukio mahakamani huitwa nini katika gazeti la *Rai*?
- 7 Je, katika magazeti hayo kuna ‘Habari za Ulimwengu’?
- 8 Je, kuna matangazo katika magazeti hayo?
- 9 Je, sehemu hiyo ya burudani inayoitwa ‘Maoni ya Washairi’ ipo katika gazeti gani?
- 10 Je, sehemu hiyo ya burudani inayoitwa ‘Michezo Katika Picha’ ipo katika gazeti gani?

# 13 Mawasiliano

## Communications

**In this unit you will learn:**

- useful vocabulary when using a telephone
- how to write letters
- how to use the neutro-passive extension **-ik-**

### Dialogue 1

*Leo's wallet is lost, so he decides to phone the police*

- 1 Where was Leo yesterday?
- 2 What suspicion does the policeman have concerning Leo's wallet?

ASKARI: (Simu inalia na askari aitika) Halo!

LEO: Je, hapa ni kituo cha polisi?

ASKARI: Ndiyo! Karibu!

LEO: Asante! Shikamoo!

ASKARI: Marahaba! Kuna nini?

LEO: Pochi yangu imepotea.

ASKARI: Imepotea au imeibwa?

LEO: Sijui. Jana nilikuwa nayo lakini leo sijui iko wapi, kwa hiyo nilikata shauri kukupigia simu.

ASKARI: Je, unakaa wapi?

LEO: Ninakaa Chuo Kikuu.

ASKARI: Je, unafanya kazi gani?

LEO: Mimi ni mwanafunzi.

ASKARI: Ulikuwa wapi jana?

LEO: Baada ya masomo, nilikwenda klabuni.

ASKARI: Labda pochi hiyo iliibwa na mchopozi.

- LEO: Jamani! Unafikiri kwamba mchopozi aliniibia pochi?  
 ASKARI: Sina hakika. Njoo kituoni ukaandike taarifa.  
 LEO: Haya, nakuja sasa hivi! Kwaheri!  
 ASKARI: Kwaheri!

## Vocabulary

<b>askari</b>	policeman, soldier, guard, warder
<b>simu</b>	telephone, telegram, telex (phone call)
<b>-lia</b>	ring (cry, weep, shout, roar)
<b>-itika</b>	reply, answer
<b>Halo!</b>	Hello! ( <i>used when answering the telephone</i> )
<b>kituo</b>	a station/stop ( <i>pl. vituo. Kituo cha polisi, Police Station</i> )
<b>pochi</b>	wallet/purse
<b>-potea</b>	get lost, go astray (wander, be ruined)
<b>-ibwa</b>	be stolen/robbed
<b>-kata shauri</b>	reach a decision, decide
<b>-pigia simu</b>	phone someone
<b>klabu</b>	club ( <i>also kilabu/vilabu, club/clubs</i> )
<b>-ibwa na</b>	be stolen/robbed by
<b>mchopozi</b>	pickpocket, purse snatcher ( <i>pl. wachopozi</i> )
<b>-ibia</b>	steal from/for, rob
<b>taarifa</b>	statement, report, announcement
<b>sasa hivi</b>	right now

## Language use

### Using a telephone

#### Simu

Telephone

#### Kuna simu hapa?

Is there a telephone here?

#### Simu iko wapi?

Where is the telephone?

#### Nataka kutumia simu.

I want to use a telephone.

**Nambari ya simu ni 8960121 (nane, tisa, sita, sifuri, moja, mbili, moja).**

The telephone number is 8960121.

**Simu inatumika./Simu inaongea.**

The line is busy.

**Simu haifanyi kazi.**

The telephone is not working.

**-piga simu**

make a call

**-pigia simu**

phone someone

**Je, ninaweza kupiga simu?**

Can I make a telephone call?

**Nitapiga simu baadaye.**

I will call later.

**Nitampigia simu kesho.**

I will call her tomorrow.

## Exercise 1

